BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWAKATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2017

# 021 KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2017

# 021 KISWAHILI

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO


DIBAJI ..... iv

1.0 UTANGULIZI ..... 1

2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI ..... 2

2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO ..... 2

2.1.1 Swali la 1: Ufahamu ..... 2

2.1.2 Swali la 2: Ufupisho ..... 8

2.2 SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA ..... 11

2.2.1 Swali la 3: Mjengo wa Tungo ..... 11

2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno ..... 15

2.2.3 Swali la 5: Utumizi wa Lugha ..... 18

2.2.4 Swali la 6: Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali ..... 21

2.2.5 Swali la 7: Mjengo wa Tungo ..... 24

2.3 SEHEMU C: UANDISHI ..... 28

2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Barua ..... 28

2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Insha ..... 32

2.4 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI ..... 37

2.4.1 Swali la 10: Maendeleo ya Kiswahili ..... 37

2.5 SEHEMU E: FASIHI KWA UJUMLA ..... 43

2.5.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi ..... 43

2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi ..... 50

2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya ..... 58

2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya ..... 66

2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Kazi za Kifasihi ..... 72

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA ..... 76

4.0 HITIMISHO ..... 76

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ..... 78

KIAMBATANISHO A ..... 79

KIAMBATANISHO B ..... 80

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Kidato cha Nne kwa somo la Kiswahili, mwaka 2017. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa walimu, wanafunzi, watunga sera, wathibiti ubora wa elimu, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya watahiniwa ni ishara inayoonesha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kuhusu mambo ambayo watahiniwa waliweza kujifunza kwa ufanisi na yale waliyoshindwa kuyaelewa vizuri.

Taarifa hii, imechambua sababu mbalimbali zilizochangia watahiniwa kujibu kwa usahihi au kushindwa kujibu maswali hayo kama ilivyotakiwa. Matokeo ya uchambuzi huu yamebainisha baadhi ya sababu zilizochangia watahiniwa kutojibu maswali kwa usahihi kama vile kushindwa kutambua matakwa ya swali, kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali katika somo na kukosa maarifa kuhusu kanuni na matumizi ya lugha kwa jumla. Uchambuzi uliofanyika kwa kila swali umebaini pia mambo yaliyosaidia watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi kama vile kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa wa mada mbalimbali katika somo, kuzingatia kanuni na matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Pia, sababu za watahiniwa kupata alama za wastani zimebainishwa hususan katika kutoa majibu yasiyojitosheleza.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kutafuta mbinu za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji ili kupata ufumbuzi wa kasoro mbalimbali zilizobainishwa katika taarifa hii. Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa maoni yaliyotolewa yakifanyiwa kazi ipasavyo, wanafunzi wanaohitimu Kidato cha Nne watapata ujuzi katika kujieleza na kufafanua dhana mbalimbali kwa ufasaha.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa wote walioshiriki kuandaa taarifa hii wakiwemo Maafisa Mitihani, Walimu na Wataalam wa TEHAMA walioshiriki katika uchambuzi huu. Baraza linatarajia kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu ili kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Kidato cha Nne kwa somo la Kiswahili kwa kipindi kingine.

Dr. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2017 kwa somo la Kiswahili. Mtihani huu ulikuwa na maswali 15 yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Matumizi ya Sarufi na Utumizi wa Lugha* mtawalia, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili* pamoja na *Fasihi kwa Ujumla*.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A, B, na D, swali moja (1) kutoka sehemu C na maswali matatu (3) kutoka sehemu E. Swali la kumi na tano (15) lilikuwa la lazima.

Mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2017 ulifanywa na watahiniwa **317,665**. Kati ya watahiniwa hao, waliofaulu ni **266,842** sawa na asilimia **84.42** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, yaani waliopata daraja A hadi D. Kiwango hicho cha kufaulu kwa jumla ni cha juu zaidi kwa asilimia **6.67** ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2016 ambapo asilimia ya waliofaulu ilikuwa **77.75.**

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na yale yaliyojibiwa vibaya katika mtihani huu. Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni *vizuri, wastani* na *hafifu*. Kiwango kizuri cha kufaulu kimeanzia alama **65** hadi **100**, kiwango cha wastani kikianzia alama **30** hadi **64** na kiwango hafifu alama **0** hadi **29**. Aidha, majedwali yenye takwimu na chati mbalimbali zimewekwa ili kufafanua viwango hivyo vya kufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya **kijani** inawakilisha kiwango kizuri cha kufaulu, rangi ya **njano** inawakilisha kiwango cha wastani na rangi **nyekundu** inawakilisha kiwango hafifu cha kufaulu. Pia, sampuli za majibu ya watahiniwa kwa kila swali zimeambatanishwa ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huo kwa kuonesha jinsi watahiniwa walivyotoa majibu yaliyokidhi/yasiyokidhi haja za maswali waliyopewa katika mtihani huu.

Uchambuzi huu utaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa ujumla wake kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika mkakati wa kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa vizazi vijavyo.

## 2.0 TATHMINI KWA KILA SWALI

Sehemu hii inafafanua uchambuzi wa kina wa kila swali na majibu yaliyotolewa na watahiniwa kwa kuonesha maswali yaliyofanyika vizuri, wastani na yale yaliyofanyika vibaya. Aidha, sababu za kufaulu kwa watahiniwa kwa kiwango cha juu, wastani au cha chini zimeelezwa bayana kwa kila swali. Sampuli za majibu ya watahiniwa kwa kila swali zimeambatanishwa ili kudhihirisha maelezo ya uchambuzi huo.

### 2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO

#### 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lilimtaka mtahiniwa kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Maswali yaligawanyika katika vipengele (a) hadi (d) vyenye jumla ya alama 5 na yalilenga kupima ufahamu wa mtahiniwa katika kusoma kifungu cha habari.


Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa aeleze sababu mbili zinazosababisha nchi mbalimbali kuhitilafiana katika muundo wake wa elimu na kilikuwa na jumla ya alama 1.

Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa afafanue namna elimu ilivyokuwa inatolewa katika jamii za kiafrika kabla ya ukoloni na kutaja waliohusika kutoa elimu hiyo na kilikuwa na jumla ya alama 2.

Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa aeleze malengo ya elimu iliyotolewa katika jamii za kiafrika na ile iliyotolewa Ulaya na kilikuwa na alama 1.

Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari kinachofaa kwa habari aliyoisoma na kilikuwa na alama 1.

Asilimia 96.76 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa kwani asilimia 81.71 ya watahiniwa hao walijibu vizuri na kupata alama za juu na za wastani. **Chati Na. 1** inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 1**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 81.71 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 5. Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 16.10 walipata alama za juu 3.5 hadi 5 kwa kuwa waliweza kujibu vizuri vipengele vingi vya swali. Aidha, watahiniwa hao waliweza kuhusisha kifungu cha habari walichokisoma katika kujibu maswali yaliyoulizwa katika kipengele (a) hadi (d) kwa usahihi. Hivyo, watahiniwa hao waliweza kueleza sababu za nchi mbalimbali kuhitilafiana katika muundo wa elimu kwa usahihi. Pia, waliweza kufafanua jinsi elimu ilivyotolewa katika jamii za kiafrika kabla ya ukoloni na kutaja watoaji wa elimu hiyo ambao ni wale waliowazidi umri au wakubwa kuliko wanaopewa elimu. Vile vile, walieleza kwa usahihi malengo ya elimu iliyotolewa katika jamii za kiafrika kuwa ni kurithisha mila za taifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuwaandaa vijana kutimiza wajibu katika nchi zao. Isitoshe, watahiniwa hao waliandika kichwa cha habari “Mfumo/Lengo la Elimu kabla ya Ukoloni” ambacho kilisadifu kwa usahihi habari waliyoisoma. Kielelezo 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi vipengele (a) hadi (c) na kupata alama za juu.

**Kielelezo 1.1**

1 (a) Sababu mbili zinazosababisha nchi mbalimbali kubadilifiana katika mwendo wake wa elimu

-> Elimu yoyote iwe ya darasani au si ya darasani ina shabaha yake.

-> Mila na desturi pia hazifanani ni tofauti tofauti.

b) i Kabla ya ujio wa ukoloni jamii za kiafrika zilikuwa zinatoa elimu ya historia za makabila yao na uhusiano baina ya kabila moja na makabila mengine. Pia walijifunza aina za majani na mizizi pamoja na kazi zake, walijifunza namna ya kushughulika na mavuno na jinsi ya kuangalia mifugo.

ii) Waliohusika katika kutoa elimu katika jamii za kiafrika walo waliokuwa na umri mkubwa katika jamii husika.


c) Elimu iliyotolewa katika jamii za kiafrika na ile iliyotolewa huko Ulaya zilikuwa na malengo ya kuimarisha mila zilizokuwa zikitumika katika nchi na kuwaandaa watoto na vijana kutimiza wajibu wao katika nchi.

d) UMUHIMU WA ELIMU

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kwa usahihi ijapokuwa, katika kipengele (d) aliandika kichwa cha habari kisichojitosheleza kwa kuandika “Umuhimu wa Elimu” badala ya “Mfumo/Lengo la Elimu kabla ya Ukoloni” na kupata alama 4.

Aidha, asilimia 65.61 ya watahiniwa waliofaulu walipata alama za wastani 1.5 hadi 3 kutokana na kutoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika vipengele mbalimbali vya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika kujibu kipengele (a) (i) alitoa sababu moja isiyo sahihi kuhusu nchi mbalimbali kuhitilafiana katika miundo ya elimu kwa kuandika "…nchi zenyewe zinazotoa elimu huhitilafiana" badala ya kujibu kuwa *mila na mazingira ya nchi ndizo hufanya miundo ya elimu kuhitilafiana*. Katika kipengele (b) (ii) mtahiniwa huyo alitoa hoja isiyo sahihi juu ya watoaji wa elimu katika jamii za kiafrika na katika kipengele (c) mtahiniwa huyo alishindwa kuelezea kwa usahihi juu ya malengo ya elimu iliyotolewa katika jamii za kiafrika na ile iliyotolewa huko Ulaya kama vile, *kurithisha mila za taifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine* (Afrika) *na kuwaandaa vijana kutimiza wajibu katika nchi zao* (Ulaya) na kupata alama za wastani. Kielelezo 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele vya swali hili na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 1.2**



1. a)
i) Kwa sababu nchi zenyewe zinazo-toa elimu huhitalijiana.
ii) Kwa sababu elimu yoyote iwe ya darasani au si ya darasani, ina shabaha yake.
b) Jamii za kiafrika zilikua zinatoa elimu kwa kuwafunza vijana kwa kushi na kutenda, walikuwafunzi uzundi wa kazi zinazopaswa ~~kutendwa~~ kufanywa na tabia zinazopaswa kwa naze watu wa jamii ile.
ii) Viongozi wa makabila ndio walio hutoka kutoa elimu katika jamii za kiafrika.
c) Elimu iliyotolewa katika jamii za kiafrika na ile iliyotolewa ilikuwa zilikua na malengo ya kuwaelimisha watu.
d) UMUHIMU WA ELIMU.

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele (a) (i), b (ii), c na kupata alama za wastani.

Aidha watahiniwa wachache, asilimia 18.29 waliojibu swali hili walipata alama 0 hadi 1 kwa kuwa walishindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kujibu vipengele (a) hadi (c) na kumudu kujibu kipengele (d) pekee kwa kuwa hakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu kifungu cha habari

alichopewa. Kielelezo 1.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kufaulu kwa kiwango cha chini.

**Kielelezo 1.3**


1. (a) (i) huhitilafiana .kwa sababu nchi nyingi zenyewe zinatoa elimu huhitalifiana elimu yeyote iwe ya darasani au si ya darasani.

(ii) kurithishana maarifa. kwa sababu mila za taifa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

(b)(i) Jamii za afrikan zilitowa elimu ya za kurithishana maarifa na mila za taifa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine

~~(ii) ulaya~~
(ii) wakoloni

(c) Elimu iliyotolewa jamii ya kiafrika ilikuwa na malengo ya kujifunza namna ya kushughulikia mazuno na jinsi ya kuangalia mifugo.


(d)

Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyojitosheleza katika vipengele vingi kutokana na kukosa ufahamu wa kutosha kuhusu kifungu cha habari alichopewa. Hali kadhalika, hakujibu maswali katika vipengele vyote kama ilivyotakiwa.

### 2.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilihusu mada ndogo ya *Ufupisho* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia maarifa ili kufupisha habari aliyoisoma. Swali lilikuwa na alama 5 na lilimtaka mtahiniwa afupishe habari kwa maneno yasiyopungua mia moja (100) na yasiyozidi mia moja na arobaini (140)

Swali hili lilijibiwa na asilimia 83.75 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Idadi kubwa ya watahiniwa (92.74%) walijibu swali hili vizuri na kufaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. **Chati Na. 2** inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 2**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Miongoni mwa watahiniwa waliojibu vizuri swali hili, wengi wao, asilimia 73.89 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3. Watahiniwa hao waliandika ufupisho usiojitosheleza hususan katika kuzingatia mpangilio wa mawazo wenye mantiki, matumizi ya alama na vituo, matumizi ya lugha sanifu, kutotumia moja kwa moja maneno yaliyotumika katika kifungu cha habari na kutozingatia idadi ya maneno ipasavyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia lugha isiyo sanifu kwa kuandika maneno "mafunza" badala ya mafunzo, "miza" badala ya mila na "hile" badala ya ile. Pia mtahiniwa huyo hakuzingatia upatanisho wa kisarufi katika baadhi ya tungo zake hasa katika aya ya mwisho mstari wa pili aliandika neno "ambayo" badala ya 'ambalo'. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la

mtahiniwa aliyeandika ufupisho usiojitosheleza na kupata alama za wastani


**Kielelezo 2.1**


2 Mwingiliano wa muundo wa elimu katika
nchi mbalimbali husababishwa na elimu elimu
yoyote hile kuwa na lengo lake katika nchi.
ambayo ni kurithisha maarifa na mila za
taifa kutoka kizazi kimoja kwenda kizazi
kingine katika jamii hunazoishi. kwahiyo
hapo zamani kabla ya ukoloni waafrika wa-
likuwa na mfumo wao wenyewe wa elimu am-
bapo wazee na watu wenye umri mkubwa
katika jamii walitoa elimu ya mafunzo kwa
vijana wao ya kuishi na kutenda ambapo:
walifundishwa tabia, ufundi mbalimbali wa
shughuli za nyumbani na pia walijifunza
namna ya kushughulika na shughuli za mauwa
na jinsi ya kuangalia mifugo.
Hivyo elimu ya ulaya na ya Afrika
zote zilikuwa na lengo moja ambayo madhumuni
yake yalikuwa ni kuimarisha mila zilizokuwa
zikitumika katika nchi.

Kielelezo 2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuzingatia baadhi tu ya taratibu za ufupisho.

Asilimia 18.85 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama 3.5 hadi 5 kutokana na kuzingatia mpangilio wa mawazo wenye mantiki, matumizi ya alama na vituo, kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini cha habari, kuzingatia idadi ya maneno na matumizi ya lugha sanifu. Kielelezo 2.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika ufupisho unaokidhi kanuni na taratibu za ufupisho kama inavyotakiwa.

**Kielelezo 2.2**


2. Ufupisho.


Mipango ya elimu hutofautiana baina ya nchi moja na nyingine. Sababu za utofauti huo ni nchi zenyewe zinazotoa elimu kuhitilafiana kadhalika na kuwa kila elimu huwa na shabaha yake. Hivyo ni uongo kuwa kabla ya ukoloni waafrika hawakuwa na elimu kwani watoto walijifunza kuishi na kutenda mfano wa mafunzo hayo ni kama mizizi na kushughulika na mifugo vilivyotolewa wa nyumbani au shambani. Hivyo wanajamii walifunzwa historia za makabila yao halikadhalika na mengine. Elimu hiyo haikupatikana darasani bali kwa watu wazima. Elimu ya Ulaya ni ya darasani na lengo lake ni sawa na ile ya Afrika. Hivyo mafunzo katika nchi nyingi hulenga kuandaa vijana wenye kuhitimika taifa lao. Hivyo, elimu inaposhindwa sehemu yoyote, hukwamisha maendeleo ya eneo hilo na watu hulalamika sana elimu yao inapowateka mpumo mbaya.

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyezingatia kanuni za uandishi na ufupisho na kupata alama za juu katika swali husika.

Watahiniwa wachache, asilimia 7.26 ndio walioshindwa kufupisha habari waliyosoma na kupata alama za chini 0 hadi 1. Watahiniwa hao hawakuzingatia taratibu za uandishi na kanuni za ufupisho kwa jumla. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alikuwa na mpangilio wa maneno usio

na mantiki, matumizi yasiyo sahihi ya alama na vituo na kutumia maneno kama yalivyo katika kifungu cha habari kwa sentensi nyingi alizotumia katika ufupisho wake. Kielelezo 2.3 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika ufupisho usiofuata taratibu na kanuni za ufupisho wa kifungu cha habari.

**Kielelezo 2.3**


2 Maisha ya watu wengi sana huaa sauliwa tuwe na elimu ya kutosha sana maana hakuna elimu yakutosha au watu hawana elimu ya kutosha kwasababu ya ukoloni wa zamani sana watu wanarudi nyuma sana kwa kawaida ya elimu hii hurudisha jamii na hata elimu ya kizamani hurudisha maendeleo nyuma kwa sababu mtu to hajomo kwa sababu ya shambo au kilimo

Kwahiyo tuna shauliwa tuwe makini katika elimu yetu hii kwa sababu ya watu wa zamani tuwe makini katika elimu hii ya kusoma au utakuwa makini sana kwa sababu ya, matokeo yote ya kielimu kuwa na maisha mazuri lazima elimu.

Kielelezo 2.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufuata kanuni na taratibu za ufupisho kwa jumla. Aidha, alitumia maneno kama yalivyo katika kifungu cha habari kinyume na utaratibu wa kufupisha habari.

## 2.2 SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

### 2.2.1 Swali la 3: Mjengo wa Tungo

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi*, mada ndogo ya *Mjengo wa Tungo* na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa aorodheshe vishazi huru katika **safu A** na vishazi tegemezi

katika **safu B** kutoka katika sentensi alizopewa na lilikuwa na jumla ya alama 5.


Swali hili lilijibiwa na asilimia 87.94 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa cha wastani ambapo asilimia 54.40 ya watahiniwa hao walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. **Jedwali Na. 1** linaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.

**Jedwali Na. 1**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa kwa Asilimia

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 - 1.0 | 127,392 | 45.60 |
| 1.5 - 3.0 | 119,587 | 42.81 |
| 3.5 - 5.0 | 32,384 | 11.59 |

Asilimia 42.81 ya watahiniwa walipata alama za wastani 1.5 hadi 3 kwa kuwa walitoa majibu yasiyojitosheleza katika kubainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kuorodhesha kwa usahihi vishazi huru katika safu A na vishazi tegemezi katika safu B katika kipengele (a) na (d), lakini katika kipengele (b), (c) na (e) aliweza kuorodhesha kwa usahihi kishazi huru na kishazi tegemezi kama ilivyotakiwa na kupata alama za wastani. Kielelezo 3.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele vingine na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 3.1**




| 3. | Vishazi huru A | vishazi tegemezi B |
|---|---|---|
| | a) Kwa kuwa imepasuka | Ngoma hailii vizuri |
| | B) Watakuja kesho | Watoto walio andikishwa. |
| | c) Amepelekewa taarifa | Kiongozi atakaye funga mkutano |
| | D) Walio wahusika | M tawa tambua |
| | E) Kina kurasa nyingi | Kitabu ulicho pewa. |

Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kupata alama za wastani.

Watahiniwa waliofaulu vizuri swali hili ni asilimia 11.59 tu ambao walipata alama za juu 3.5 hadi 5. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vishazi katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeorodhesha kwa usahihi vishazi huru katika safu A na vishazi tegemezi katika safu B.

**Kielelezo 3.2**



3. Kuanisha vishazi huru na vishazi tegemezi


| Safu A (Huru) | Safu B (tegemezi) |
|---|---|
| a) Ngoma hailii vizuri | - kwa kuwa imepasuka |
| b) Watakuja kesho | - Watoto walioandikishwa |
| c) Amepelekewa taarifa. | - kiongozi atakayefunga mkutano |
| d) Mtawatambua | - Waliowasikivu. |
| e) Kina kurasa nyingi. | - kitabu ulichopewa. |

Kielelezo 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuorodhesha kwa usahihi vishazi huru katika safu A na vishazi tegemezi katika safu B katika sentensi alizopewa.

Asilimia 45.60 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu 0 hadi 1 kutokana na kushindwa kuorodhesha vishazi huru

katika safu A na vishazi tegemezi katika safu B katika sentensi walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alikosa vipengele vyote vitano yaani (a) hadi (e) kwa kushindwa kubainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi alizopewa na kupata 0 kutokana na kukosa maarifa kuhusu dhana ya vishazi katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo 3.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyechanganya vishazi huru na vishazi tegemezi katika safu moja huku akivunja tungo hizo na kuzifanya kusomeka kwa neno moja moja kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 3.3**



| 3 | SAFU A | SAFU B |
|---|---|---|
| a) | Ngoma | Hailii |
| | Kiwa | Imeparuka |
| | Vizuri | |
| | Kuwa | |
| | | |
| b) | Watoto | walioandikishwa |
| | Kesho | watakuja |
| | | |
| c | Kiongozi | atakayefunga |
| | | Mkutano |
| | | Amepelekewa |
| | | taarifa |
| | | |
| d | Walio | Watawatambua |
| | wasikivu | |
| | | |
| e) | Kitabu | ulichopewa |
| | Kurasa | kina |
| | Nyingi | |

Kielelezo 3.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuorodhesha vishazi huru (safu A) na vishazi tegemezi (safu B) na badala yake akavunja sentensi hizo katika neno moja moja.


### 2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na mada ndogo za *Aina za Maneno*. Swali lililenga kupima uchambuzi na liligawanyika katika vipengele (a) na (b). Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya kielezi kisha kutoa mfano wa sentensi moja na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kubainisha kielezi katika kila tungo aliyopewa, kisha kutaja aina ya kielezi husika. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 5.

Kiasi cha watahiniwa 304,939 sawa na asilimia 95.99 kati ya wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha kufaulu ambapo, asilimia 61.95 walipata alama za wastani na zaidi na kulifanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi.

Watahiniwa wengi (133,885) sawa na asilimia 43.91 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3. Watahiniwa hao walishindwa kutoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele vya swali hili ambapo baadhi waliweza kubainisha vielezi katika tungo walizopewa, lakini walikuwa hawana maarifa kuhusu aina za vielezi hivyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kubainisha vielezi katika tungo na kutaja aina za vielezi kwa usahihi katika vipengele 4 (b) (i) na (ii); na kushindwa katika kipengele (b) (iv) na 4 (a). Kielelezo 4.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi tu ya vipengele na kushindwa vingine.

**Kielelezo 4.1**


04. a) Kielezi

Ni maneno ambayo yanaelezea juu ya kitu fulani au mahali fulani

Mfano:

Mama analima shamba

K E

Shamba - Kielezi

b)

i) Darasani kuna utulivu mkubwa

E

Kielezi cha mahali

ii) Wanafunzi wanaimba kimasihara

E

Kielezi kinacho onyesha utani (kutotilia maanani

iii) Mwalimu amerudi tena

E

Kielezi kinacho eleza wakati (muda / njeo)

(iv) Nitaondoko wiki inayokuja

E


Kinaeleza wakati ujao.

Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebaini kwa usahihi vielezi na aina zake kwa baadhi ya vipengele na kushindwa kubaini katika vipengele vingine.

Kiasi cha watahiniwa 55,021 sawa na asilimia 18.04 walijibu vizuri swali hili na kupata alama 3.5 hadi 5 kutokana na kueleza kwa usahihi maana ya *kielezi* na kutoa mfano wa sentensi moja. Vile vile, waliweza kubainisha vielezi kwa kuvipigia mstari katika kila tungo na kutaja aina ya kielezi husika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza maana ya kielezi na kutoa mfano mmoja kama ilivyotakiwa. Vilevile, mtahiniwa huyo aliweza kubainisha kwa usahihi kielezi katika tungo

na kutaja aina za vielezi hivyo na kupata alama zote 5. Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali.


**Kielelezo 4.2**


4. Kielezi - Ni maneno yanayoeleza jinsi namna tendo linavyo tendeka
mfano. Kinyonga anatembea polepole
polepole - Kielezi cha namna au jinsi E
E
(i) Darasani - Kielezi cha mahali
E
(ii) kima sahara - cha namna au jinsi
E
(iii) tena - Kielezi cha Idadi
E

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali husika kwa usahihi.

Aidha, watahiniwa 116,033 sawa na asilimia 38.05 kati ya watahiniwa wote waliojibu swali hili, walipata alama za chini (dhaifu) 0 hadi 1 kwa kuwa hawakuweza kutoa maana sahihi ya *kielezi* na mfano wake na wengine kushindwa kubaini vielezi katika tungo na kutaja aina za vielezi hivyo. Miongoni mwao, watahiniwa 43,038 sawa na asilimia 14.11 walipata 0 kwa kuwa walishindwa kujibu maswali katika vipengele vyote. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana na mfano wa kielezi ambao sio sahihi na kupigia mstari vitenzi katika tungo alizopewa badala ya vielezi. Kielelezo 4.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo 4.3**


4(a) Kielezi, Ni aina ya neno ambayo huonyesha utenda au mdedwa wa jambo fulani. Mfano alinicheka sana. hapo kielezi ni alinicheka,

4(b) i/ Darasani kunautulivu Mkubwa
- Kielezi cha ~~[illegible]~~ Sifa.

4(b) ii/ Wanafunzi wanaimba kimasihara
- Kielezi cha wakati

4(b) iii/ Mwalimu amerudi tena
- Kielezi cha tendo

4(b) iv/ Nitaondoka wiki inayokuja
- Kielezi cha wakati

Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha vitenzi badala ya vielezi katika sentensi alizopewa kinyume na matakwa ya swali.


### 2.2.3 Swali la 5: Utumizi wa Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* na mada ndogo ya *Utata Katika Mawasiliano* na lililenga kupima matumizi. Swali lilimtaka mtahiniwa atoe maana tano tofauti za neno “kibao” kisha atunge sentensi moja kwa kila maana aliyotoa. Swali lilikuwa na jumla ya alama 5.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 95.49 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi ambapo asilimia 77.84 walipata alama za juu na za wastani yaani alama 1.5 hadi 5. Kati yao, asilimia 58.95 walijibu swali hili kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama 1.5 hadi 3. Watahiniwa hao walitoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa maana tatu za neno “kibao” kwa usahihi na kutunga sentensi sahihi kulingana na maana hizo, lakini maana nyingine alizotoa

hazikuwa sahihi na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 5.1**


5. (i) kibao
Ni kifaa kinachotumika kujingea au
Ni Ubao wa mbao itiwa ni kipini cha mbao.
Mfano. Juma leta kile kibao.
(ii) Ni kifaa kilichoandikiwa maneno kwa ajili ya kufahamisha mahali fulani.
Mfano: Aiba amepita katika Hospitali ya ocean road kwa kuangalia kibao.
(iii) Hutumika kuonyesha tendo limefanyika mara ngapi.
Mfano! Ali amepigwa mara nyingi zaidi ya mara moja.
(iv) Hutumika kuonyesha kipigo ambacho mtu amepigwa.
Mfano. Amina amechapwa kibao cha kofi, lilia paa!
(V) Sehemu ndogo ya kuandikia kwa chaki.


Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine na kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 18.89 ya watahiniwa waliojibu vizuri na kupata alama 3.5 hadi 5 waliweza kutoa maana tano tofauti za neno ‘kibao’ kisha wakatunga sentensi moja kwa kila maana. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa maana tano tofauti za neno ‘kibao’ kwa usahihi kama vile;

> “…kifaa cha kuandikia, kikalio kisicho na kiegemeo, kipande cha ubao kwa ajili ya shughuli maalum, mbuzi ya kukunia nazi, kifaa cha kufyatulia matofali, kipigo cha kiganja cha mkono, muziki, kibao cha matangazo….”

Katika maana hizo zilizotolewa, mtahiniwa huyo aliweza kutunga sentensi sahihi zilizoendana na maana alizotoa. Kwa mfano, maana mojawapo ya kibao aliyotoa ni "*kipande cha mbao kilichoandikwa maandishi fulani yanayotoa taarifa*" na sentensi aliyotunga kuhusu maana hiyo ni "*Yupo karibu na kibao cha shule*". Kielelezo 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 5.2**



05 Maana za neno "kibao"

(a) Kifaa kwaajili ya kujengea
Mfano: Aliweka kibao kidogo dirishani.

(b) Kifaa cha kukunia nazi
Mfano: Niletee kibao cha nazi

(c) Kwaajili ya kuukumia chapati
Mfano: Kaniazimie kibao cha chapati


(d) Kipande cha mbao kilichoandikwa maandishi fulani yanayotoa taarifa.
Mfano: Yupo karibu na kibao cha shule.

(e) Kumuadhibu mtu kwa kumpiga na kiganja cha mkono
Mfano: Alipigwa kibao na mwalimu.

Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutoa maana sahihi tano za neno "kibao" na kuweza kutunga sentensi nzuri kulingana na maana zilizotolewa.

Fauka ya hayo, asilimia 22.16 ya watahiniwa walipata alama dhaifu 0 hadi 1 kutokana na kushindwa kutoa maana tofauti za neno "kibao" na na kutunga sentensi kwa kila maana. Aidha, asilimia 4.32 ya watahiniwa hao walipata 0 kwa kushindwa kabisa kutoa maana ya neno 'kibao' na kutungia sentensi maana hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana ya "kibao" kama vile; *Kibao ni" kipisi cha mbao", "ni kipisi cha ubao ", " ni kipisi cha kiti" na "ni kipisi cha meza"* na sentesi zilizotungwa hazikuwa na uhusiano wowote na maana husika ya neno "kibao". Kielelezo 5.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo 5.3**





Kielelezo 5.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili kwa kutoa majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swali.

### 2.2.4 Swali la 6: Matumizi ya Lugha Katika Miktadha Mbalimbali

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na mada ndogo ya *Misimu*. Swali lililenga kupima maarifa ambapo mtahiniwa alitakiwa kutoa mfano mmoja wa misimu zagao iliyovuma Tanzania katika vipindi vifuatavyo; (a) Muda mfupi baada ya kupata uhuru, (b) Miaka ya Azimio la Arusha, (c) Njaa ya mwaka 1974/ 1975, (d) Miaka ya vita vya Kagera na (e) Kipindi cha hali ngumu ya maisha baada ya vita vya Kagera. Swali lilikuwa na jumla ya alama 5.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 229,586 sawa na asilimia 72.27 kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Aidha, swali hili linaongoza kwa kuwa na kiwango kidogo zaidi cha kufaulu ambapo idadi ndogo sana ya watahiniwa yaani asilimia 1.35 pekee ndio waliofaulu na

kupata alama za juu na za wastani. **Chati Na. 3** inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na. 3**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa wengi sana, asilimia 98.65 walijibu vibaya swali hili na kupata alama 0 hadi 1 kutokana na kushindwa kubaini misimu zagao iliyovuma Tanzania katika vipindi tofauti kama vile *muda mfupi baada ya Uhuru*, *miaka ya Azimio la Arusha*, *njaa ya mwaka (1974/1975) na kipindi cha vita vya Kagera*. Miongoni mwao, asilimia 91.60 walishindwa kabisa kujibu swali hili na kupata 0. Kiwango cha chini cha kufaulu kwa watahiniwa hawa kinadhihirisha kuwa hawakuwa na maarifa kuhusu misimu zagao iliyovuma Tanzania katika vipindi vilivyotajwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika neno moja lenye kuwakilisha vipindi hivyo vivyotajwa badala ya misimu zagao iliyozuka katika vipindi hivyo kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 6.1**

6. a) Muda mfupi baada ya kupata uhuru
- Ukombozi.

b) Miaka ya Azimio la Arusha
- Ujamaa.

c) Njaa ya mwaka 1974/1975.
- Kuhemea.


d) Miaka ya vita vya Kagera.
- Mapambano.

e) Kipindi cha hali ngumu ya maisha baada ya vita vya kagera.
- Umaujiki.

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali kwa kutoa majibu yasiyohusu misimu zagao iliyovuma Tanzania katika vipindi tofauti tofauti vya kihistoria alivyopewa.

Aidha watahiniwa wachache sana, asilimia 1.35 pekee ndio waliojibu swali hili na kufaulu kwa kiwango cha juu (0.06%) na cha wastani (1.29%). Watahiniwa hao, licha ya kuwa na maarifa kuhusiana na misimu hiyo, pia walielewa vizuri matakwa ya swali hili na kumudu kutoa mifano ya misimu zagao katika vipindi vilivyotajwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa kwa usahihi mifano ya misimu zagao iliyotumika katika vipindi vifuatavyo: *Muda mfupi baada ya kupata uhuru*, *Miaka ya Azimio la Arusha*, *Njaa ya mwaka 1974/1975*, *Miaka ya vita ya Kagera* na *Kipindi cha hali ngumu ya maisha baada ya vita ya Kagera.* Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa kufuata matakwa ya swali kwa usahihi japokuwa alikuwa na tatizo la kiuandishi kwa baadhi ya maneno kama vile…'wakajuwa' badala ya 'wakajua' na pia alikata maneno mengi isivyostahili kama vile 'kuli-zushwa' badala ya 'kulizushwa' na mengineyo.

**Kielelezo 6.2**


6
(a) Wana hili wali ambiwa kuwa wanatakiwa kulinda uhuru na ndipo walijua kuwa uhuru ni kazi
(b) Kuli kuwa na kauli iliyotumika kwa mtu unyonyaji au usiwe kupe
(c) Kuli zushwa maneno kama ya muhi hali na kangata Malindi ya yanga na unga wa njano
(d) Wananchi waliambiwa wafunge mikanda kutokana na hali ya njaa na wengine walijitolea ngombe na vyakula
(e) wali tumia neno ndali kama mtu gaidi katika kilimani dada,


Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali kwa kuweza kutoa mfano wa misimu zagao iliyovuma Tanzania katika vipindi vilivyotajwa kwa ufasaha na uweledi wa kutosha.

### 2.2.5 Swali la 7: Mjengo wa Tungo

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na mada ndogo ya *Mjengo wa Tungo* na lilihusu miundo ya kiarifu. Swali lililenga kupima maarifa na lilikuwa na vipengele viwili ambapo kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa aeleze maana ya kiarifu na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kwa kutumia mifano, ataje miundo minne ya kiarifu. Swali lilikuwa na jumla ya alama 5.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 82.40 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Aidha, swali hili pia ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha chini cha kufaulu ambapo watahiniwa wachache, asilimia 27.81 pekee ndio waliokuwa na kiwango cha wastani na cha

juu cha kufaulu. **Chati Na. 4** inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 4**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Idadi kubwa ya watahiniwa, asilimia 72.19 walikuwa na kiwango cha chini na kupata alama 0 hadi 1 kutokana na kushindwa kueleza maana sahihi ya kiarifu na kutaja miundo yake kama ilivyotakiwa. Miongoni mwao, asilimia 40.06 walipata 0 kutokana na kushindwa kabisa kueleza maana ya kiarifu na kutaja miundo ya kiarifu. Majibu ya watahiniwa hao yalionesha dhahiri kuwa, hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mjengo wa tungo unaotumia *kiima* na *kiarifu*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kutoa maana ya kiarifu kwa kuandika kuwa "*Kiarifu ni neno ambalo halijitoshelezi kimaana linapokuwa mwenyewe*". Vilevile, alitaja miundo minne ya kiarifu kama; *muundo huru, muundo wa moja kwa moja, muundo wa kawaida na muundo wa utatanishi* majibu ambayo si sahihi. Mtahiniwa alitakiwa kutaja miundo ya kiarifu ifuatayo:

> Prediketa au Kifungu Tenzi (KT); Kikundi Kitenzi (KT) na Kikundi Nomino (KN); Kikundi Nomino (KN) na Kikundi Kielezi (KE); Kikundi Kitenzi (KT), Kikundi Nomino (KN) na Kikundi Kielezi (KE).

Aidha, mtahiniwa huyo alitoa mifano isiyokidhi miundo ya kiarifu katika tungo. Kielelezo 7.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana ya kiarifu na kutaja miundo yake.


**Kielelezo 7.1**


7 (a) Kiarifu ni neno ambalo halijitosholezi
Kimaana linapokuwa mwenyewe
mfano, Sana na pia ni neno lenye mapu-
ngufu katika maana yake na pia
hata umbo wake haujitosholezi
Kimantiki
(b) Miundo ya kiarifu
(i) Sana muundo huu
mfano (i) Yupi ni mzuri
(ii) Yupi tena
(ii) Muundo wa moja kwa moja
mfano (i) ni wewe Asha
(ii) mbona hupatikani
(iii) Muundo wa kawaida
mfano (i) Mani kaja
Mani anataka
(iv) Muundo wa utafanishi
mfano (i) Mani karimia
Mani katelekezwa

Kelelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kutoa majibu sahihi katika kuelezea maana ya kiarifu na miundo minne ya kiarifu.

Watahiniwa wachache, asilimia 6.19 pekee ndio waliojibu swali hili vizuri na kupata alama za juu za kufaulu 3.5 hadi 5, kwa kuwa waliweza kueleza kwa ufasaha maana ya kiarifu na kutaja miundo minne ya kiarifu kwa usahihi na kutoa mifano dhahiri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi maana ya kiarifu kuwa ni *sehemu ya sentensi inayokaliwa na vitenzi*. Pia alitaja miundo minne ya kiarifu kama vile "*kitenzi peke yake"*, *"kitenzi na shamirisho*", "*kitenzi na chagizo*" na *kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu"* na aliweza kutoa mifano sahihi inayoendana na miundo ya kiarifu aliyoitaja na kupata alama za juu. Kielelezo 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kuzingatia matakwa ya swali.

**Kielelezo 7.2**



7. a) Kiarifu ni sehemu ya sentensi inayotaliwa na kikundi cha vitenzi. Mara nyingi kiarifu hutokea upande wa kulia wa sentensi mbele ya Kiima. ~~Vitenzi na~~ nomino na vielezi huweza kujitokeza.

b) Miundo minne ya kiarifu.

i) Kitenzi peke yake.
mfano: Haruna / anakula.
T

ii) Kitenzi na shamirisho.
mfano: Ana / anaimba wimbo.
T Sh.


iii) Kitenzi na chagizo.
mfano: Johni / anakimbia barabarani.
T Ch.

iv) Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu.
mfano: Musa / alikuwa anaandika
Ts. T

Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi maana ya kiarifu na kutaja miundo minne ya kiarifu na kutoa mifano sahihi.

Hata hivyo baadhi ya watahiniwa, asilimia 21.62 walipata alama za wastani kuanzia 1.5 hadi 3 kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya vipengele vya swali hili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana ya kiarifu isivyo kwa kuandika "*ni sehemu ya tungo/neno linaelezea zaidi kuhusu mtendwa au mtendwa wa jambo fulani*" badala ya kueleza kuwa ni 'sehemu ya sentensi inayotoa taarifa juu ya jambo linalofanywa na kiima'. Vilevile, katika muundo wa kiarifu aliweza kutaja miundo mitatu kwa usahihi na kushindwa muundo mmoja ambapo aliandika, *muundo wa nomino na kivumishi* ambao sio sahihi. Katika kipengele 7 (b) (i), (ii) na (iii) aliweza kutaja miundo ya kiarifu na kutungia mifano sahihi. Kielelezo 7.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 7.3**


7. (a) Kiarifu (A) ni sehemu ya tungo/neno linaolezea zaidi kuhusu mtendwa au mtendwa wa jambo fulani.

(b) (i) Muundo wa kitenzi
Mfano:
Mama na baba wanalima.
A

(ii) Muundo wa kitenzi na kielezi
Mf: Kaka na dada walitembea haraka haraka.
A

(iii) Muundo wa kitenzi na kitenzi kisaidizi.
Mfano: Kaka alikuwa analia.
A

(iv) Muundo wa nomino na kirumishi.
Mfano: Mama ana kiatu cheupe.
A

Kielelezo 7.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele na kushindwa katika vipengele vingine.

## 2.3 SEHEMU C: UANDISHI

### 2.3.1 Swali la 8: Uandishi wa Barua

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi wa Barua,* mada ndogo ya *Uandishi wa Barua za Kirafiki* na lililenga kupima uundaji. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10 na lilimtaka mtahiniwa kuandika barua kwa rafiki yake kuhusu mipango yake baada ya kumaliza Kidato cha Nne ambapo jina lake lilitakiwa liwe Dito Jito wa S.L.P 300 Longido na jina la rafiki yake liwe Kijito Bahari wa shule ya Sekondari Mtaweza S.L.P 200 Dar es salaam.


Swali hili lilijibiwa na asilimia 70.29 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kilikuwa kizuri ambapo watahiniwa wengi (73.61%) walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani na kulifanya swali hili kuwa mojawapo ya maswali yaliyojibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa. **Jedwali Na. 2** linaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.

**Jedwali Na. 2**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 - 2.5 | 58,930 | 26.39 |
| 3.0 - 6.0 | 56,491 | 25.30 |
| 6.5 - 10.0 | 107,864 | 48.31 |

Asilimia 48.31 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifanya vizuri na kupata alama za juu 6.5 hadi 10 kutokana na kuandika barua ya kirafiki kwa usahihi. Watahiniwa hao waliweza kuandika barua kwa kuzingatia anuani ya mwandishi (kona ya juu kulia), tarehe ya barua (chini ya anuani ya mwandishi), mwanzo wa barua, kiini cha barua, salamu za maagano na jina la mwandishi. Pia walizingatia matumizi sahihi ya alama, vituo, aya na lugha sanifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuandika barua ya kirafiki kwa kuzingatia kanuni na taratibu zote za uandishi kama ilivyotakiwa. Kielelezo 8.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika barua ya kirafiki vizuri kulingana na matakwa ya swali na kupata alama za juu.

**Kielelezo 8.1**



8.

Shule ya Sekondari Mtaw[illegible]
S.L.P 200,
Dar-es-Salaam.

31 oktoba, 2017.

Mpandwa Dito,

Salaam. Natumaini umzima wa afya kwani mimi niko salama na naendelea vyema.

Lengo la barua hii ni kukueleza kuhusu mipango yangu pindi nitakapomaliza shule ya sekondari kidato cha nne. Ninapanga kwenda kumsalimu bibi na babu yangu na kuwasaidia shughuli za shamba kwani nina hamu ya kujua jinsi ya kulima, kuvuna na kupanda.

Pia nitakwenda kujifunza kozi mbalimbali hasa za upishi na jinsi ya kutumia kompyuta kwani utandawazi wetu unazidi kukua. Vilevile nitakwenda mbuga za wanyama mbalimbali kwani nataka kujifunza kuhusu wanyama.

Ni matumaini yangu nitapokea barua kutoka kwako ikinieleza juu ya mipango yako. Wasalimu wote ndugu na marafiki zako.


Ni mimi rafiki yako,
Kijito Bahari.

Kielelezo 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kufuata vigezo vyote vya uandishi wa barua ya kirafiki ikiwa ni pamoja na matumizi sahihi ya taratibu na alama za uandishi.

Aidha, asilimia 25.30 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani 3 hadi 6 kutokana na kutozingatia baadhi ya kanuni za uandishi wa barua za kirafiki ipasavyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika barua bila kuonesha salamu za maagano, lengo la barua, pia mawazo yake hayakupangika vizuri. Aidha, matumizi ya lugha sanifu na alama za uandishi kama vile vituo, mkato na aya havikuzingatiwa katika uandishi wake. Pia katika mwanzo wake wa

barua (upande wa kushoto) alianza kwa herufi ndogo neno *“ndugu”*. Kielelezo 8.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika barua ya kirafiki na kuzingatia baadhi ya kanuni na kupata alama za wastani.

**Kielelezo 8.2**


8.

SHULE YA SEKONDARI MTAWEZA,
S.L.P 200,
Dar-es-Salaam,
31.10.2017.


ndugu rafiki Dito Jito,
Kwanza napenda kukusalimu kwajila la yesu, ni matumaini yangu kwamba unaendelea vizuri na shughuli zako za kimasomo Mimi pia naendelea vizuri na ninakaribia kuanza mtihani wangu wa kidato cha nne wiki ijayo. Lengo la barua hii ni kukujulisha kuwa baada ya mtihani wangu wa taifa ningependa tufanye kama tulivyo kuwa tumepanga.
Ningeomba kabla sijaja huko uandae lile shamba ambalo tulipanga kwenda kulima kwa lengo la kupata fedha za kuendelea na kidato cha tano mwakani
Sina mengi ya kusema zaidi ya kuomba ushirikiano wako.
Asante
Wako mtiifu
Kijito Buhari

Kielelezo 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kuandika barua ya kirafiki isiyojitosheleza kwa baadhi ya vigezo vya uandishi wa barua ikiwa ni pamoja na matumizi ya herufi ndogo mwanzoni mwa sentensi kama vile “*ndugu…*”badala ya Ndugu…

Aidha, watahiniwa wachache, (26.39%) walishindwa kuandika kwa usahihi barua ya kirafiki na kupata alama 0 hadi 2.5. Miongoni mwao, asilimia 22.28 walishindwa kabisa kuandika barua ya kirafiki kutokana na kukosa maarifa kuhusu muundo wa barua hiyo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika barua ya kikazi kwa kuweka anwani mbili yaani anwani ya mwandishi na mwandikiwa, kichwa cha barua, mwisho wa barua ya kikazi, sahihi ya mwandishi, na cheo cha mwandishi kinyume na matakwa ya swali. Mtahiniwa alitakiwa kuandika barua ya kirafiki akizingatia muundo kama vile:- *anuani ya*

*mwandishi (katika kona ya juu kulia), tarehe (chini ya anuani), Mwanzo wa barua (upande wa kushoto), Kiini cha barua, salamu za maagano, jina la mwandishi pamoja na kuzingatia matumizi ya alama, vituo, aya na matumizi ya lugha sanifu.* Kielelezo 8.3 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeandika barua ya kikazi badala ya barua ya kirafiki.

**Kielelezo 8.3**



8.

SHULE YA SECONDARY MTAWEZI,
S.L.P 200.
DAR-ES-SALAAM.

30/10/2017.

DITO JITO,
S.L.P 300,
LONGIDO.

Ndugu;

YAH: MIPANGO YANGU YA BAADAYE NITAKAPOMALIZA KIDATO CHA NNE

Rejea na mada tajwa hapo juu ni matumaini yangu yakuwa wewe ni mzima wa afya kwa upande wangu mi ni mzima na naendelea vizuri na mitihani yangu.

Nitakapomaliza kidato cha nne nina mipango mingi sana ambayo nitaifanya rafiki yangu. kwanza kabisa nitakuja kutembelea pia nitakuwa mimi pamoja na rafiki yangu wa kiume pia napenda sana nitakapomaliza nicheze karakoshi pamoja na simu mpaka matokeo yangu yatakapotoka.

Hayo ndiyo baadhi ya malengo yangu nitakapomaliza kidato cha nne naimani yatakuwa umeyapenda na kuyafurahia.

Wako mtiifu.

Kijito Bahari
(Mwanafunzi).


Kielelezo 8.3 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeandika barua ya kirafiki kwa kutumia muundo wa barua ya kikazi kinyume na matakwa ya swali.

### 2.3.2 Swali la 9: Uandishi wa Insha

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi wa Insha* na mada ndogo ya *Uandishi wa Insha za Hoja* na lililenga kupima uundaji. Swali hili lilimtaka mtahiniwa aandike insha ya hoja isiyopungua maneno 250 na

isiyozidi maneno 300, kuhusu "Madhara ya madawa ya kulevya nchini Tanzania" na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache (92,094) sawa na asilimia 28.99% pekee kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, kwa kuwa lilikuwa swali la kuchagua. Aidha, swali hili lilijibiwa vizuri sana ambapo asilimia 96.79 walipata alama za juu na za wastani za kufaulu. **Chati Na. 5** inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.





**Chati Na. 5**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 62.39 ya watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walipata alama za juu (6.5 hadi 10) kutokana na kuwa na uwezo wa kuandika insha kwa ufasaha na kwa usahihi kwa kuzingatia kanuni na taratibu zote za uandishi wa insha. Watahiniwa hao waliweza kuandika kwa usahihi kichwa cha insha na utangulizi mzuri kuhusu "Madawa ya kulevya", na katika kiini waliweza kuelezea madhara ya madawa ya kulevya kama vile; Kupungua kwa nguvu za uzalishaji mali, kudhoofisha kinga ya mwili na kusababisha udhaifu wa mwili, kuongeza kasi ya maambukizi ya Kifua Kikuu na UKIMWI, kuwafanya watumiaji wake kujihusisha na maswala ya uhalifu kama vile wizi/ujambazi, kuleta mifarakano miongoni mwa wanafamilia na kuongezeka kwa vifo/umaskini kwa mtu mmoja mmoja na Taifa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kichwa cha insha kwa herufi kubwa na kuandika utangulizi mzuri unaoeleza watumiaji wa madawa hayo na kutaja baadhi ya aina za madawa ya kulevya kama vile:- *Bangi*, *kokein* pamoja na *mirungi*. Pia katika kiini, mtahiniwa huyo alielezea kwa usahihi madhara ya madawa ya kulevya kama

ilivyotakiwa na kufaulu kwa kiwango cha juu. Aidha mtahiniwa huyo aliweza kuzingatia taratibu za uandishi, matumizi ya lugha sanifu, idadi ya maneno na kutoa hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo 9.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika insha vizuri kwa kuzingatia vigezo vyote muhimu vya uandishi wa insha.

**Kielelezo 9.1**



MADHARA YA MADAWA YA KULEVYA TANZANIA;

Swl.9 Madawa ya kulevya ni madawa yanayotumiwa na watu kwa sababu ya kujiperahisha wenyewe. Mfano bangi, kokeini pamoja na mirungi. Madawa haya huwa na madhara kama yafuatayo;

Mtu anayetumia madawa ya kulevya hupata magonjwa mbali mbali kama vile saratani ya Mapafu na damu hivyo huweza kumpelekea kifo.


Pia, mtu anayetumia madawa ya kulevya katika makamo ya uwanafunzi ina mpelekea ~~ach~~ aache kwenda shuleni sababu ya kupuuzia masomo darasani na kuwa kupoteza ndoto zake ~~maishani~~ maishani.

Kutokana na madawa ya kulevya hii hupelekea ongezeko la matendo ya wizi na ubakaji. Katika matendo ya ubakaji ~~wizi~~, madawa huharibu akili hupelekesha ~~mtu~~ akili hivyo mtu hupanya kile ambacho anajisikia kufanya kama vile kubaka mtu hali kadhalika wizi hutokana na kutafuta hela kwa njia yoyote ilimpate madawa yake

Kielelezo 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali kwa kuweza kuandika insha ya hoja kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa insha kiufasaha.

Miongoni mwao, asilimia 34.40 walipata alama za wastani 3 hadi 6 kwa kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa utangulizi usiojitosheleza na kufafanua ‘madhara ya madawa ya kulevya’ kwa hoja dhaifu. Aidha, mtahiniwa huyo hakuzingatia taratibu za uandishi wa insha ipasavyo kama vile matumizi ya herufi kubwa na vituo kama ilivyotakiwa. Kielelezo 9.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielezo 9.2**


9\. MADHARA YA MADAWA YA KUL
EVYA.
Madawa ya kulevya huleta madha
ra katika jamii madhara hayo ni kama
kifo, kubambikiwa uzazi, kusababisha umas
kini suala la madawa ya kulevya
[illegible] ujangiwe [illegible] katika ja
mii [illegible] jamii [illegible] na kuleta
maendeleo katika nchi
Yafuatayo ni madhara ya madawa
ya kulevya
Husababisha kifo - ni mojawapo ya madha
ra ya madawa ya kulevya inayoikumb
a jamii suala la utumiaji wa madawa
ya kulevya [illegible] [illegible] katika
nchi yetu ya Tanzania
Kuharibika kisaykolojia - katika
utumiaji wa madawa ya kulevya pia hu
sababisha mtu kuharibika kisaykolojia
na kutokujielewa. Viongozi wanatakiwa kuje
nga jamii kwa kukemea suala la utumia
ji wa madawa za kulevya
Chanzo cha ugonvi katika fami
lia. ni chanzo cha ugonvi endapo baba au
mama anatumia dawa za kulevya
Huharibu uzazi/kizazi - pia kati
ka suala la utumiaji wa madawa za kul
evya huweza kuleta madhara katika uzazi

Kielezo 9.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza na pia kutozingatia tahjia ya baadhi ya maneno ipasavyo kama vile '*kisaykolojia, ugonvi*'…badala ya kuandika kisaikolojia, ugomvi n.k.

Aidha, watahiniwa wachache sana, asilimia 3.21 walishindwa kuandika insha kutokana na kukosa maarifa ya uundaji wa insha kwa jumla. Baadhi ya watahiniwa, (0.73%) walipata alama 0 kwasababu baadhi yao walibadilisha kichwa cha insha na kutumia vingine kinyume na matakwa ya swali. Wapo waliotunga hotuba na wengine kuelezea jinsi ya kupambana na madawa ya kulevya kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga insha kuhusu "ATHARI ZA UGONJWA WA UKIMWI" huku akielezea namna ugonjwa wa huo unavyoweza kuambukizwa kutoka kwa mtu

mmoja kwenda kwa mwingine ”badala ya kuandika kuhusu “MADHARA YA MADAWA YA KULEVYA NCHINI TANZANIA” kama ilivyotakiwa. Aidha, katika hitimisho lake alishauri serikali itoe elimu juu ya UKIMWI na athari zake ili kuzuia usambaaji wake. Kwa ujumla mtahiniwa huyo hakuelewa matakwa ya swali kwani alitumia kichwa cha insha ambacho hakupewa. Kielelezo 9.3 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 9.3**

9. ATHARI ZA UGONJWA WA UKIMWI

Ukimwi ni upungufu wa Kinga mwilini, ugonjwa huu uliingia Tanzania mnamo miaka ya Themanini, inasemekana ugonjwa huu ulitokea uganda ukapitia Kagera na kusambaa nchi nzima.

Ugonjwa huu husambaa kwa njia mbalimbali kama vile kujamiana bila kutumia kondomu, kuchangia vitu vyenye ncha kali kama vile viwembe, sindano na hata pini. Pia ugonjwa huu huweza kuambukizwa kwa mama kwa mtoto pia vilevile kumshika mwathirika wa ukimwi kwenye majeraha ikiwa na wewe mwinguzi unamajeraha mikononi au sehemu yoyote ya mwili wako. Pia ugonjwa huu unaweza kuambukizwa kwa kushea mdomo kati ya mume na mke kwani mmoja kati yao kama anaugonjwa huu huweza kumuambukiza mwenzake.

Njia za kupambana na ugonjwa huu ni kutumia kinga kama vile kondom wakati wa kujamiana au kuwa na mpenzi mmoja ambaye ni mwaminifu katika suala la mapenzi.


Kielelezo 9.3 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga insha kuhusu “**Athari za Ugonjwa wa Ukimwi**” badala ya “Madhara ya Madawa ya Kulevya” kama ilivyotakiwa.

## 2.4 SEHEMU D: MAENDELEO YA KISWAHILI

### 2.4.1 Swali la 10: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*. Swali lililenga kupima tathmini na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kuwa lugha ya Kiswahili imetokana na lahaja za kibantu kwa kueleza hoja mbili kuhusu chanzo cha lahaja na hoja tatu kuhusu matumizi ya lahaja katika lugha ya Kiswahili. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Asilimia 70.85 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha chini na watahiniwa wengi. **Chati Na. 6** inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 6**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*


Watahiniwa wengi (65.50%) walijibu vibaya swali hili na kupata alama za chini 0 hadi 2.5. Kati yao, asilimia 44.54 walipata 0 kwa kuwa walishindwa kabisa kueleza chanzo cha lahaja kama vile:

> *Utengano wa kijiografia kati ya jamii moja na nyingine* na *utengano wa kitabaka uliotokana na uchumi, dini, elimu au siasa uliokuwepo katika jamii fulani ya kibantu ulisababisha kuwa na vilugha tofauti.*

Aidha, walishindwa kueleza matumizi ya lahaja katika lugha ya Kiswahili kama vile:- "*kupamba lugha, kukuza lugha pamoja na kuonesha mitindo mbalimbali ya wazungumzaji katika lugha*". Kwa

mfano, mtahiniwa mmoja badala ya kueleza chanzo cha lahaja alielezea chimbuko la Kiswahili kuwa ni kibantu kwa kutoa hoja za *kihistoria na kiisimu* na kwa upande wa matumizi ya lahaja ya Kiswahili alitoa hoja kama vile:- "*Ngeli za nomino, mnyumbuliko wa vitenzi na msamiati*", majibu ambayo si sahihi. Kielelezo 10.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo 10.1**


10 Kibantu ; ni Maeneo ambayo
yanasibitika kuwa ndiyo chimbuko la kiswa-
hili katika kuenea na kukuwa nchini.
Afrika. kuelezea chanzo cha lahaja k .
katika lugha ya kiswahili imetoo-
kana na lahaja za kibantu kwa hoja
zifuatazo
Kihistoria ; katika historia.
tunaona kuna watu walisaidii kugundua kuwa
kiswahili ni kibantu ambapo walikuja.
watu mbalimbali kwa Mfano Al - Idrisi
ambapo Mtu huyu alikuja maeneo ya
unguja mnamo karne ya 10 ambapo ali
sibitisha kuwa kiswahili ni kibantu na
pia Mtu mwengine Marco huyu nae alikuja
Maeneo ya pemba au unguja na mwisho
ni Tanzi
Kiisimu ; katika kiisimu tu
naona kuwa na kusibitisha kuwa kiswa
hili ni kibantu kwa sababu kulikuwa
na mpatanisho wa vitenzi au mnyumbuli
ko ambapo walipeleke baazi ya makabila
kulinganisha vitenzi vya kiswahili na lug
ha za makabila .
Na pia lahaja ilitumika .
katika Matumizi katika kiswahili kwa
hoja zifuatazo
Ngeli za nomino ; katika
Matumizi ya lahaja katika kiswahili
kulikuwa na Ngeli za nomino ambazo
zilibainisha kuwa kiswahili ni kibantu
katika aina nyingi za Ngeli za nomi

Kielelezo 10.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeelezea chimbuko la Kiswahili kama chanzo cha lahaja na kutoa hoja zisizo sahihi katika kueleza matumizi ya lahaja.

Aidha, kwa upande wa watahiniwa waliofanya vizuri swali hili, asilimia 8.23 pekee ndio waliojibu vizuri na kupata alama za juu 6.5 hadi 10. Watahiniwa hao waliweza kuthibitisha kuwa lugha ya Kiswahili imetokana na lahaja za kibantu, kwa kueleza hoja mbilli kuhusu chanzo kama vile *utengano wa kijiografia na kuwepo kwa matabaka* na hoja tatu kuhusu matumizi ya lahaja katika lugha ya Kiswahili zilizohusisha hoja kama *kupamba lugha*, *kukuza lugha pamoja na kuonesha mitindo mbalimbali ya wazungumzaji katika lugha*". Kielelezo 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja chanzo cha lahaja na kutoa maelezo sahihi kuhusu matumizi ya lahaja katika lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo 10.2**

10.

Lahaja, Ni tofauti zilizopo kati ya lugha moja au zaidi kimaana, kimuundo, kimantiki na kimatamshi. Lahaja hutokea katika wazungumzaji wa lugha kuu moja na kuwatofautisha kimaana, kimuundo, kimantiki na kimatamshi katika lugha yao kuu moja.

Ni kweli kwamba lugha ya Kiswahili imetokana na lahaja za Kibantu. Lahaja hizi zilitokea kutokana na sababu tofautitofauti katika jamii.

Zifuatazo hoja zielezeazo chanzo cha lahaja kutokea katika lugha.


**Utengano wa kijiografia;** lahaja huweza kutokea pale watu wanaoishi katika eneo moja wakatofautishwa na kisiwa, kilima au mabonde, watu hawa hutofautiana katika ~~moja~~ matumizi ya lugha kwani wale wanaishi katika eneo moja hata matumizi, misamiati, matamshi na muundo wa lugha utafanana.

**Kuwepo kwa Matabaka;** Kuwepo kwa matabaka mbalimbali katika jamii vilevile huchochea lahaja kuwepo kwani kila tabaka litakuwa na matumizi yake ya kilugha hata katika lugha ya Kiswahili, watu ~~wenye~~ walio katika tabaka moja eidha kidini au kisiasa mara nyingi matumizi yao ya kilugha kimuundo, kimaana, kimantiki na kimatamshi hufanana.

Mbali na vyanzo, lahaja pia ina matumizi katika Kiswahili sanifu.

Zifuatazo ni hoja kuhusu matumizi ya lahaja katika Kiswahili sanifu.

**Kupamba lugha;** lahaja hupamba lugha kwani kupitia lahaja lugha hupata maumbo mbalimbali kutoka katika jamii mbalimbali.



10. Kukuza lugha; lahaja vilevile hukuza lugha kwani katika maeneo tofauti maneno mbalimbali ambayo yenye maana sawa au tofauti huzalishwa na hivyo lugha huzidi kukua kimsamiati na hivyo lugha inakua zaidi.

Kuonesha mitindo mbalimbali ya uzungumzaji katika lugha; kupitia lahaja kwa kuwa katika maeneo tofauti kunakuwa na lahaja tofautitofauti na hivyo katika haya maeneo uzungumzaji huwa ni tofauti kutokana na lahaja na hivyo lugha kuwa na mitindo mbali mbali ya uzungumzaji.

Hivyo basi, lahaja ina umuhimu katika kukuza msamiati pamoja na hayo kuna vitu vinavyo kwamisha kukua kwa lahaja navyo ni; ~~kuongezeka,~~ kuendelea kwa njia za upashaji habari, usanifisha, kuendeleoa kwa njia za usafiri na vilevile ni kuwepo chini ya utawala mmoja.

Kielelezo 10.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kuweza kueleza chanzo sahihi cha lahaja na kuelezea matumizi sahihi ya lahaja katika lugha ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, asilimia 26.27 ya watahiniwa walipata alama za wastani 3 hadi 6 kutokana na kutoa majibu yasiyo sahihi kwa baadhi ya hoja kuhusu chanzo cha lahaja na matumizi yake katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea chanzo cha lahaja kwa kutoa hoja kama vile;.. *kutaka kuongeza msamiati katika lugha”* na *“lahaja kuwa na historia kutumia lugha moja”* majibu yasiyo sahihi, lakini akaweza kueleza matumizi ya lahaja katika lugha ya Kiswahili kama vile:- “*hukuza lugha, hupamba lugha* na *husanifisha lugha*”, majibu ambayo ni sahihi. Hata hivyo, aliweza kutoa hitimisho zuri linaloendana na matakwa ya swali na kupata alama za wastani. Kielelezo 10.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 10.3**

10. Lahaja ni utofauti mdogo uliopo kati lugha ya mazingira fulani na lugha ya nyingine katika kimatamshi, kimsamiati, kimuundo na maumbo. lahaja ina aina nyingi kipemba, kiunguja, kimrima na kimtangata. Lahaja ni lugha iliyotokana na lugha za kibantu. kuthibitisha kauli hii kwa kutoa hoja kuelezea chanzo cha lahaja na matumizi yake katika kiswahili.


Lahaja ni kutaka kuongeza msamiati katika lugha; Lahaja ya kiswahili inachukukua maneno kutoka lahaja nyingine ili kukamilisha au kuongeza msamiati wa neno na kulifanya liwe na maana zaidi. Msamiati wa neno unakuwa katika eneo pana na kupata watumiaji wengi zaidi. mfano lahaja ya Unguja, kipemba

Lahaja kuwa na historia ya kutumia lugha moja; lahaja inatumia lugha za kibantu ili kukamilisha maana na kuweza kukua na kuenea kwa kiasi kikubwa kwa watumiaji wengi. mfano lahaja ya kiunguja na kiungwana.

Yafuatayo ni matumizi ya lahaja katika kiswahili Sanifu.

Kukuza lugha; lahaja imetumika kukuza lugha kutoka na watumiaji kuwa wengi wanayosaidia kukuza na kueneza kiswahili Sehemu nyingi nchini. Lahaja za kibantu zimesaidia sana kukuza lahaja katika maeneo mbalimbali. Mfano. Lahaja ya kipemba na Kikongo.

Kupamba lugha; lahaja imetumia maneno mengi ya kibantu kupamba ili iweze kuwa lugha fasaha. Kutokana na Ubantu maneno mengi yanafanana na lugha ya kiswahili. Hivyo wanayachukua na kuyasanifisha ili kupata msamiati mpya. mfano kiswahili maji kisukuma minze.



10. Kusanifisha Lugha; Kutokana na lahaja ya kiswahili lugha inasanifishwa na kuwa lugha fasaha ambayo inaweza kutumika katika jamii inayotuzunguka. Lugha ya kibantu kama kiunguja, kikongo wanayachukua maneno na kuyasanifisha ili kupata misamiati mipya. Mfano Lahaja za Kongo, Kiunguja.

Mambo yote niliyoyataja yanaeleza chanzo na matumizi ya lahaja katika kiswahili. Lahaja inahitaji kukuzwa na kuenezwa kwa sehemu mbalimbali ili iweze kuwa na misamiati mingi. Na kuwe na watu wanaosaidia kuikuza, kuwe na wataalamu wengina Vifaa vya kutendea kazi.


Kielelezo 10.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa hoja zisizo sahihi kuhusu chanzo cha lahaja na kutoa hoja sahihi kuhusu matumizi ya lahaja katika lugha ya Kiswahili.

## 2.5 SEHEMU E: FASIHI KWA UJUMLA

### 2.5.1 Swali la 11: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Njia za Kuhifadhi Fasihi Simulizi*. Swali lililenga kupima uchambuzi na lilimtaka mtahiniwa kufafanua changamoto nne zinazoweza kujitokeza kwa kuhifadhi Fasihi Simulizi katika maandishi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na zaidi ya nusu ya watahiniwa (59.71%) kati ya wote waliofanya mtihani japokuwa lilikuwa swali la kuchagua. Watahiniwa wengi (85.51%) walipata alama za juu na za wastani na kulifanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi. **Chati Na. 7** inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 7**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 48.47 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama 10 hadi 15 kwa kuwa waliweza kufafanua kwa usahihi changamoto nne zinazoweza kujitokeza kwa kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uwasilishwaji wa fasihi kwa njia ya maandishi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika majibu yake aliweza kutoa utangulizi mzuri unaoendana na swali na katika kiini aliweza kufafanua kwa usahihi changamoto nne zinazojitokeza kwa kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi kama vile:- "*uwepo wa gharama" , "humilikiwa na wachache ", "itapoteza utendaji wake"* na *"fanani na hadhira hawataonana*" , hoja zinazopatikana katika aya ya i, ii, iii na ya iv. Vile vile, mtahiniwa huyo alitoa hitimisho zuri linaloendana na swali. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 11.1**

11. Fasihi simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia lugha kufikisha ujumbe pamoja na masimulizi ya mdomo. Fasihi simulizi imegawanyika katika vipengele kama hadithi, semi, sanaa za maonyesho na ushairi. Kutokana na umuhimu wa fasihi simulizi huitaji kuhifadhiwa njia mojawapo ni njia ya maandishi. Njia ni nzuri ingawa hupoteza uhai na uhalisia wa fasihi simulizi. Zifuatazo ni changamoto zinazoweza kujitokeza kwa kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi.

Kwanza kabisa, uwepo wa gharama ni changamoto moja wapo inayojitokeza kwa kuhifadhi fasihi simulizi katika maandisha. Endapo fasihi simulizi itahifadhiwa katika maandisha itawalazimu watu kuingia kwenye gharama kwa kutafuta hela na kusaka sehemu vitu hivi vinauzwa. Lakini fasihi simulizi ikihifadhiwa kichwani itakuwa rahisi kwa kila mmoja kupata na kufanikisha alitakalo.

Itamilikiwa na wachache endapo fasihi simulizi ikihifadhiwa katika maandishi. Fasihi simulizi haitaji ujuzi wowote hivyo kila mtu watubwa kwa wadogo ni rahisi kuipata. Lakini endapo fasihi simulizi itahifadhiwa kwa njia ya maandishi wenye uwezo wa kusoma na kuandika ndiyo watakao faida yaani wasomi ingawa wengine wasiojua kusoma watahathirika. Hivyo ni changamoto nyingine inayoweza kutokea endapo fasihi simulizi itahifadhiwa kwenye maandishi.

Itapoteza utendaji wake endapo fasihi simulizi ikihifadhiwa katika maandishi. Fasihi simulizi huhusisha utendaji. Yaani fanani na hadhira hushiriki

11· ipasavyo. Hii inaweza kumuhuisha fanani anaimba, akionyesha matendo nao hadhira wakichota, wakipiga makofi na kushangilia. Sasa endapo itahifadhiwa katika maandishi fasihi simulizi itamhusisha msomaji mwenye hivyo utendaji hutapotea. Hivyo basi upoteaji wa mtendaji ni changamoto nyingine.

Fanani na hadhira hawataonana endapo fasihi simulizi itahifadhiwa kwa njia ya maandishi. Fasihi simulizi inamuhusisha fanani ambaye ni mtambaji na hadhira ambaye ni msikilizaji au mtazamaji endapo fasihi hii itawasilishwa kwa njia ya maandishi fanana na hadhira watapotea yaani hawataonana. Hapa msomaji hatashiriki pamoja na msikilizaji hivyo changamoto.

Kwa kuhitimisha, fasihi simulizi isihifadhiwa kwa njia ya maandishi kwani ni ya gharama, hupoteza utendaji, humilikiwa na wachache na fanani na hadhira hupoteana. Njia mbadala ziletwa ili changamoto hizi zisitumike hivyo tupate kuendeleza utamaduni wetu.

Kielelezo 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua vizuri changamoto za kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi, japokuwa alikuwa na makosa machache ya kisarufi katika aya ya pili kwenye neno "hamilikiwa" badala ya kuandika *humilikiwa.*

Aidha, asilimia 37.04 ya watahiniwa walipata alama za wastani 4.5 hadi 9.5 kutokana na kufafanua kwa usahihi baadhi ya changamoto za kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi, kutoa utangulizi na hitimisho lisilojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika utangulizi alieleza *maana ya fasihi* badala ya kuelezea maana ya fasihi simulizi kama swali lilivyotaka. Pia, alifafanua hoja isiyo sahihi kama vile "fasihi simulizi ikihifadhiwa katika maandishi huweza kuibiwa". Aidha, changamoto nyingine alizifafanua kwa usahihi na kupata alama za wastani. Kielelezo 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 11.2**

11 Fasihi ni sanaa itumiayo lugha ili kufi-
kisha ujumbe wake kwa watu husika. Ku
na aina mbili za fasihi ambazo ni fasihi sim-
ulizi na fasihi andishi. Fasihi andishi huhifa-
dhiwa na zifuatazo ni changamoto zikumbaza uhifa
dhi wake
Gharama: Kuhifadhi kazi ya fasihi sim
ulizi katika maandishi ni gharama mfano
kuchapisha kazi ya fasihi na kuhifadhi hum
gharimu mtu pesa ndefu ambayo hi huweza
kuwa changamoto
Huweza kuibiwa: Kazi ya fasihi simulizi
iliyowekwa kwa njia ya maandishi huwe-
za kuibiwa na kusababisha kupotea kwa
kazi hiyo muhimu ya kisanaa yenye
manufaa katika jamii
Huteketea au kuharibika: Kazi ya fasihi
simulizi iliyo katika mfumo wa maandishi
huweza kuteketea au kuharibika pale
sehemu ulipoihifadhia mfano makazi
kuungua na moto hivyo basi kusababisha
upotevu wa kazi hiyo ya kisanaa
Hupotea; Kazi ya fasihi simulizi
iliyokatika mfumo wa maandishi pia hu
weza kupotea kama itakuwa imehifadhi-
wa kwenye vifaa kama kompyuta, amb-
ama vifaa hivyo vikiharibika husababi
sha hata kazi hiyo ya fasihi kupotea.
Fasihi ni bora na muhimu katika
jamii na uhifadhi wa kazi hizi za kis-
ana uwe wenye umakini ili zisije potea.

Kielelezo 11.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani, kwa kuweza kutoa majibu sahihi kwa baadhi ya hoja na kushindwa kufafanua hoja nyingine.

Watahiniwa wachache, (14.49%) pekee ndio waliojibu vibaya kwa kutoa majibu yaliyo kinyume na matakwa ya swali na kupata alama dhaifu 0 hadi 4. Baadhi yao, asilimia 2.12 tu ndio walionekana kukosa maarifa kabisa kuhusu changamoto za kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi na kupata 0. Watahiniwa hao walitakiwa kufafanua changamoto kama;

> kupotea kwa utendaji, kutokuwepo kwa kiimbo, fanani na hadhira hawaonani, kutokupokea mabadiliko ya papo kwa hapo, ni mali ya mwandishi,wanaofaidika ni wanaojua kusoma tu na inaweza kupotea kwa urahisi.

Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliweza kutoa utangulizi mzuri na kushindwa kabisa kufafanua changamoto za kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi kwa kuandika, "*mtu hawezi kusahau maneno yaliyoandikwa, inaweza kuweka kumbukumbu, haipotezi muda tukiwa tuna simulia hadithi na fasihi simulizi muda mwingine maneno anayotamka msimulizi huwa hazileti maana*". Kielelezo 11.3 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili.

**Kielelezo 11.3**

11 Fasihi Simulizi ikihifadhiwa katika maandishi hupoteza uhai na uhalisia wake fafanua changamoto nne zinazo weza kujitokeza kwa kuhifadhi fasihi Simulizi katika maandishi.

Fasihi Simulizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo. fasihi Simulizi inaweza kuwa hadithi, ngojera, nyimbo. changamoto za fasihi Simulizi ni kama ifuatayo.

fasihi Simulizi ikihifadhiwa kahika fasihi andishi mtu hawezi kusahau maneno yaliyoandikwa. maneno hayo yatamsaidia kupata elimu tofauti na kujiandaa vizuri kama akiwa na kitu cha kusema kwa jamii.

Inaweza kuweka kumbukumbu kama vile ukitumia fasihi Simulizi ukaambiwa urudie tena itakuwa ngumu kwasababu baadhi ya maneno mtu anaweza kusahau lakini aki hifadhi kwenye fasihi aandishi ata kumbuka maneno yote.


haipotezi mdaa tukiwa tunasimulia hadithi watoto wana weza kuchoka kusikiliza lakini kama hadithi hiyo ikiaandikwa kwenye vitabu na tukaweka picha watoto watafurahi kusoma vitabu hivyo.

Kielelezo 11.3 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili kwa kushindwa kufafanua changamoto sahihi za kuhifadhi fasihi simulizi katika maandishi japokuwa katika utangulizi wake aliweza kutoa maana sahihi ya fasihi simulizi.

### 2.5.2 Swali la 12: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Ushairi*) na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kujadili kauli kuwa, "msanii ni kinda la jamii husika hivyo anayoandika huihusu jamii hiyo" na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wachache, (34.35%) kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa swali la kuchagua. Watahiniwa wengi (94.81%) walijibu vizuri na kupata alama za juu na za wastani. **Chati Na. 8** inaonesha viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia.





**Chati Na. 8**: *Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia*

Asilimia 69.40 ya watahiniwa waliopata alama za juu 10 hadi 15 waliweza kujadili kauli kuwa '*msanii ni kinda la jamii na aandikayo huihusu jamii hiyo*' kwa kutoa hoja tatu sahihi kwa kila diwani kutoka katika diwani mbili walizosoma. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika majibu yake alitoa utangulizi mzuri unaoendana na matakwa ya swali, na kutoa hoja kwa kutumia diwani ya "*Malenga Wapya*" na "*Wasakatonge*".

Katika diwani ya "*Malenga Wapya*" mtahiniwa aliweza kuonesha jinsi msanii alivyo kinda la jamii yake kwa kuyaweka wazi mambo yaliyopo katika jamii kama vile:- "Uongozi mbaya, umuhimu wa kutumia pesa vizuri na maadili." Katika diwani ya "*Wasakatonge*"

alitoa hoja kama vile:- “kupiga vita rushwa, tabia ya uzembe na unafiki”. Mtahiniwa huyo aliweza kufafanua hoja zake vizuri na kutaja majina ya mashairi yenye kutoa ujumbe husika. Vile vile aliweza kunukuu baadhi ya beti za mashairi hayo ili kuthibitisha kile alicho kieleza katika hoja zake na kutoa hitimisho zuri linaloendana na matakwa ya swali. Kielelezo 12.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri.

**Kielelezo 12.1**


12. Msanii ni mzaliwa/mkazi wa
jamii anayoishi na maandishi/usanii wake uendana
na jamii anayoishi msanii huyo. hivyo basi mambo
yaliyoandikwa na wasanii mbalimbali ndiyo yanayo-
tokana na maisha ya jamii husika. Kwa kutumia
diwani ya "MALENGA WAPYA" pamoja na
"WASAKATONGE". zifuatazo ni hoja zinazoonesha
kuwa msanii ni kila la jamii husika.
Kwa kuanza na diwani ya "MALENGA
WAPYA" zifuatazo ni hoja. Uongozi mbaya: Katika
jamii tunaishi na viongozi wa nyanja mbalimbali
Serikali, dini, elimu. lakini viongozi wengi hawana
nyota ya uongozi kwani wao badala ya kuleta
maendeleo wao husaidia kudumaza kwa ~~kupitia~~
njia ya kujinafsisha wenyewe. Hawawaonei huruma
watu wanaoteseka kwa kutumia shairi la
Payuka mwandishi anasema.

12. "Kupayuka kwenu huko,
Mbona tu kokoriko,
Sioni unalokua".

Msanii ameonesha kuwa katika jamii yake kuna viongozi wa serikali wanaoahidi vitu vingi wakati wa kuomba kula lakini wakilisha pewa kura hawatekelezi walichoahidi.

Umahimu wa kutumia pesa vizuri: pesa ni muhimu na nzuri endapo imetumika vizuri kwani italeta mabadiliko. lakini kuna watu ambao hawajali matumizi mazuri ya pesa mwandishi wa shairi la Israfu anasema.

"Israfu ikimea,
Mali inayoyoma,
Watu watakuzomea,
Ukikosa egemea".

Msanii ameonesha kuwa ni bora mtu atumie mali vizuri kwani hiyo mali ikilisha watu watadharau na kusema hata ya uongo. hivyo basi anawaalika watu watumie vizuri pesa.

Maadili: kuna maadili mazuri na maadili mabaya. maadili yanayotakiwa ni yale yaliyo mazuri kwani ndio chanzo cha maendeleo. Katika jamii ya leo utalipwa kulingana na maadili uliyo nayo. Kwa kutumia shairi la Hisani halipwa mwandishi anasema.

"Akuulizaye uwapo na shida,
Akuteteaye unaposhambuliwa,
Akumulikaye uwapo na giza,
Hisani halipwa".

Mwandishi anaamini kuwa chochote unachotenda mtu kwa mwenzake naye atatendewa hivyo hivyo

12. hata kama hatakua yuleyule aliyetendewa. Hivyo tunaaliKwa kutenda yaliyo mema ili tulipwe mema.

Kwa kutumia diwani ya "WASAKATONGE" mwandishi ameonesha Rushwa: rushwa ni tatizo kubwa katika ulimwengu huu kwani watu wengi huaribu mali nyingi kwa sababu ya rushwa kwa upande wao huona wamepata faida. Shairi la Klabu linadhibitisha.

"Tupige vita rushwa,
Juhudi kuzifufua,
Kazi kuheshimiwa"

Msanii ameona kwa upande wake rushwa imekuwa chanzo kikubwa kwa juhudi za watu kushuka kwani mtu hatafanya juhudi zozote kwani anakua kuwa atatoa rushwa. hivyo msanii anashauli watu kufufua juhudi zao ili kuleta maendeleo.

Uzembe: uzembe ni moja ya tabia zinazorudisha maendeleo nyuma mwandishi ameona uzembe kwa watu wengi ambao kazi yao ni kufanya starehe na wakati kazi hafanyi. mwandishi wa shairi la Klabu linadhibitisha.

"Si Klabu ya usawa,
Imejaa shakawa,
Dhamiri ya kuua".

Klabu imesimama kama jamii kwa jamii nyingine watu wake ni wazembe hasa viongozi ambao wanategemea wananchi wake kulipa kila kitu wakati wao hawasaidii katika kujenga Taifa na jamii kwa ujumla.

Kielelezo 12.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kueleza bayana mambo yaliyopo katika jamii yaliyoandikwa na wasanii wa diwani teule japokuwa nukuu yake katika aya ya tatu kwenye diwani ya " Wasakatonge" haikuwa sahihi.

Asilimia 25.41 ya watahiniwa waliofaulu pia katika swali hili walipata alama za wastani 4.5 hadi 9.5 kutokana na kutoa hoja zisizojitosheleza katika kujadili kauli kuwa, "msanii ni kinda la jamii yake, yote aandikayo huihusu jamii hiyo". Aidha wengine walitoa hoja sahihi lakini walishindwa kuzitolea maelezo na mifano kutoka katika diwani husika ili kushadidia maelezo hayo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa utangulizi usioendana na matakwa ya swali. Vivyo hivyo, alitaja hoja sahihi bila ufafanuzi wa kutosheleza mahitaji ya swali kwa mfano, hoja ya pili katika diwani ya "*Malenga Wapya*" aliandika;

> "Hupiga vita Unyonyaji.- hii imejidhihirisha katika shairi la "*Punda*" limeonesha jinsi gani punda anavyo nyonywa na kuonewa"

Mtahiniwa huyo hakueleza jinsi unyonyaji huo unavyofanyika na ushauri juu ya swala hilo. Vilevile, alitaja mashairi yasiyoendana na dhima ya baadhi ya hoja alizotoa. Kwa mfano, katika diwani ya "*Wasakatonge*" mtahiniwa alitoa hoja ya "kupiga vita ukoloni mamboleo" lakini akafafanua hoja hiyo kwa kutumia shairi la "*Wanawake Wa Kiafrika*" linalozungumzia ukombozi wa mwanamke kinyume na dhima ya kupiga vita ukoloni mamboleo. Kielelezo 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 12.2**

| | |
|---|---|
| 12 | Msanii, nimtu anae ~~anae~~ haliki kazi |
| | ya fasihi. Kwa kutumia diwani ya |
| | "MALENGA WAPYA" iliyo andikwa na ~~Mohamed S.~~ Takiraki |
| | ~~Khatibu~~ mwaka 2006 na diwani ya |
| | "WASAKATONGE" iliyo andikwa na Mohamed S. |
| | Khatibu kujadili kauli isemayo "Msanii ni |
| | kinda la jamii husika hiyo anayoandika huihu |
| | su jamii hiyo". |
| | Kwa kuanza na diwani ya "MALENGA |
| | WAPYA" kujadili kauli isemayo "Msanii |
| | ni kinda la jamii husika hiyo anayoandi |
| | ka huihusu jamii hiyo kwa hoja zifuata |
| | zo |

Hupiga vita matabaka; Ni tabaka la chini ambalo lino nyonya na hii imeji dhihilisha katika shahili la "Samaki wa kutu goni" kinaonesha jinsi gani samaki anavyo nyonya

Hupiga vita unyonyaji; Hii imejidhihi lisha katika shairi la "punda" limeonesha jinsi gani punda anavyo nyonya na kuonewa

Hupiga vita umaskini; hii imeji dhihilisha katika shairi la "Mkulima" Mkulima amewekwa katika tabaka la hali ya chini sana.

Kwa kufuatia na diwani ya "WAJAKATONGE" kudhihiti kauli isemwayo "Msanii ni kinda la jamii husika hivyo anacho andika huihusu jamii hiyo kwa hoja zifuatazo

12 Hupiga vita ukoloni mamboleo; hii ime jitokeza katika shairi la "WANA WAKE WA KIAFRIKA" imejidhihilisha jinsi gani wana wake wa Kiafrika wanavyo onewa.

Hupiga vita uongozi mbaya; hii ime jitokeza katika shairi la "HISAFU" imeonesha jinsi gani viongozi wanavyo tumia madaraka vibaya. hii ata katika jamii yetu ya sasa kuna viongozi ama wanatumia ~~daet~~ madaraka vibaya.

Hupiga vita unyanyasaji, hii ime jitokeza katika shahili la "WAJAKATONGE" limeonesha jinsi gani wajakatonge wana vyo nyanyaswa


Hivyo; Msanii katika jamii ana cho kiandika ni kweli kinahusika jamii hiyo.

Kielelezo 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kutokana na kuwepo kwa mapungufu katika baadhi ya majibu yake.

Aidha, watahiniwa wachache sana (5.19%) walishindwa kujibu swali hili na kupata alama za chini 0 hadi 4. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha katika uchambuzi wa maudhui katika shairi hivyo kushindwa kujadili ni jinsi gani msanii alivyo kinda katika jamii yake kwa kuandika yaliyopo katika jamii hiyo. Hata hivyo, asilimia 2.66 walipata 0 kwa kuwa walishindwa kabisa kuchambua maudhui katika diwani teule na badala yake walitumia vitabu teule vya riwaya au tamthiliya kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitumia Riwaya ya "*Takadini*" na *Watoto wa Mama N'tilie*" kujadili dhamira zilizojitokeza badala ya kujadili kauli ya "msanii ni kinda la jamii yake, yote aandikayo huhusu jamii hiyo" katika diwani mbili alizosoma. Kielelezo 12.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua dhamira zilizopo katika Riwaya ya "*Takadini*" na "*Watoto wa Mama N'tilie"* badala ya kutumia diwani mbili alizosoma kujadili kauli ya kuwa "msanii ni kinda la jamii yake, yote aandikayo huhusu jamii hiyo" kwa kutoa hoja tatu kwa kila diwani.

**Kielelezo 12.3**

| | |
|---|---|
| 1a | Dhamira: Ni lengo la mwandishi ulilo |
| | kusudia katika kazi ya fasihi ili kufiki- |
| | sha ujumbe kati ya wanajamii. Mwandi- |
| | shi huandika mambo yanayohusu jamii. |
| | Kwa kurejelea katika diwani mbili am- |
| | bazo ni "TAKADINI" uliyo andikwa na mwandishi |
| | BEN HANSON na diwani ya "WATOTO WA MAMA - |
| | N'TILIE" uliyo andikwa na EMMANUEL MBOGO ya- |
| | fuatayo ni mambo yaliyo kusudiwa kuandikw- |
| | a na msanii kwa kuanzia na diwani ya - |
| | "TAKADINI" |
| | Malezi ya watoto. Mwandishi amejaribu |
| | kugusia suala la malezi ya watoto katika |
| | jamii ambapo amechora mwanamke kama |
| | mlezi na msimamizi mkuu katika malezi ya |
| | watoto mwandishi amemchora sekai kama |
| | mama bora lakini pia katika jamii yetu - |
| | wanawake wamekuwa wakishughulika na malezi. |


Kwa kurejerea diwani ya WATOTO WA MAMA NTILIE mwandishi ameandika yale yanayo ihusu Jamii yetu ya sasa.

Umasikini; Mwandishi amejaribu kujadili suala la umasikini ambapo jami ya mama ntilie imekubwa na kushindwa kutekeleza wajibu ipasavyo hivyo imepelekea mama ntilie na mzee Lomolomo kushindwa kulipia ada ili watoto wao waendelee na masomo lakini pia katika jamii yetu tunakubwa na umasikini ambao unapelekea hali mbaya katika maisha.

Madawa ya kulevya na ulevi. Lakini pia mwandishi amegusia suala la matumizi ya madawa ya kulevya mwandishi amemchora muhusika peter ambaye amejiingiza katika makundi mabaya ya uvutaji wa bangi aki shawishiwa na rafiki yake musa katika jamii yetu matumizi ya madawa ya kulevya yamelete maafa makubwa kama, wizi, uto na kushuka kwa kiwango cha elimu.

Migogoro Mwandishi amegusia suala la migogoro kama chanzo cha umasikini kupitia muhusika Lomolomo amekuwa chanzo cha migogoro katika familia yake kwasababu ya ulevi katika Jamii yetu migogoro imekuwa ni chanzo cha umasikini.

Hivyo basi wasanii wanajaribu kutoa uozo uliopo katika jamii kupitia kazi za kifasihi ili tuweze kutatua matatizo mbalimbali.

Kilelezo 12.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali kwa kutumia riwaya na kujadili dhamira mbalimbali badala ya kujadili kauli aliyopewa kwa kutumia diwani mbili alizosoma.

### 2.5.3 Swali la 13: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Riwaya*) na lililenga kupima matumizi. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua usemi usemao “Elimu ni ufunguo wa maisha” kwa kutoa hoja tatu kutoka katika kila kitabu katika vitabu viwili vya riwaya kati ya riwaya teule, na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi na watahiniwa wengi. Asilimia 81.80 walipata alama za wastani na za juu kuanzia 4.5 hadi 15.

Miongoni mwa watahiniwa hao, asilimia 47.94 walipata alama za wastani 4.5 hadi 9.5 kutokana kufafanua baadhi ya hoja kwa usahihi na nyingine kuzitolea maelezo yasiyojitosheleza kuelezea usemi “Elimu ni ufunguo wa maisha”. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika majibu yake alitumia riwaya ya “*Watoto wa Mama N’tilie*” pamoja na “*Takadini*”. Katika riwaya ya “*Watoto wa Mama N’tilie*”, hoja yake ya kwanza haikuwa sahihi kwa sababu alielezea athari zinazotokana na ulevi badala ya kuelezea jinsi gani mtu akikosa elimu huweza kupata athari mbalimbali zikiwepo ulevi wa pombe, wizi na fikra potovu. Aidha, hoja nyingine alizotoa hazikuwa na maelezo toshelevu na pia alikuwa na makosa ya kisarufi kwa kuandika neno *“ugambazi*” badala ya ujambazi, *“mwana”* badala ya mwanae. Aidha mtahiniwa huyo pia alichanganya dhana ya Riwaya na Tamthiliya kwa kuandika *Tamthia*” akimaanisha tamthiliya. Vile vile, katika riwaya ya “*Takadini*” mtahiniwa huyu alijadili dhamira bila kuhusisha na usemi “Elimu ni ufunguo wa maisha” na hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 13.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa wa aina hiyo.

**Kielelezo 13.1**

13 Elimu ni ujuzi anaoupata mtu kuhusu jambo fulani. Nikweli kuwa Elimu ni ufunguo wa maisha. Kauli hii inathibitishwa kwakutumia Riwaya mbili kati ya TAKADINI kilicho andikwa na Ben. J. Hanson na WATOTO WA MAMA NTILIE kilicho andikwa na E. mbogo.

Kwakuanza na Riwaya ya WATOTO WA MAMA NTILIE mwandishi wa riwaya hii amejalibu kuonyesha njinsigani. Elimu ni ufunguo wa maisha kama ifuatavyo.

Hutoa athali zipatikanazo katika suala nzima la Ulevi, kwamfano tuna muona musika mzee ~~mitor~~ Lomolomo ambaye alikuwa akilewa mpaka anasahau majukumu yake ya kikazi.

Hutupilia mbali wizi, ugambazi na uzaji wa madawa ya kulewa. kwamfano tuna waona wahusika, kama pita na musa kwasababu ya ukosefu wa Elimu. ilipelekea kujilngiza katika tabia mbaya za ujambazi.

Kutoa ujinga na huwafanya watu - waelimike, mfano kwakumuangalia muhusika mama mazoe ni ujinga alio kuwano ulio mfanya kupoteza kwa maisha ya niwana zita kwa kuto jua - athali zipatikanazo baada ya kung'atwa na - mbwa mwenye kichaa.

Sambamba na Tamthia ya WATOTO WA MAMA NTILIE PIA katika Tamthia ya - TAKADINI mwandishi wa riwaya hii amejalibu kuonyesha njinsigani ni ufunguo wa maisha kama ifuatavyo.

Kwa kupiga vita mila na desturi zilizo pitwa na wakati, kwamfano, kuamini kuwa

Kielelezo 13.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa majibu na ufafanuzi wa hoja usiojitosheleza kulingana na matakwa ya swali.

Watahiniwa wengine (33.86%) walipata alama za juu 10 hadi 15 kwa kuwa waliweza kufafanua kwa usahihi usemi "Elimu ni ufunguo wa maisha", na kuelezea jinsi elimu inavyowakwamua watu kutoka katika matatizo mbalimbali yaliyopo katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kufafanua usemi huo kwa kutoa utangulizi mzuri unaowiana na swali kwa kuelezea maana ya elimu na katika kiini cha swali, mtahiniwa huyo alitumia riwaya ya "*Takadini*" na "*Watoto wa Mama N'tilie*"kwa kutoa hoja kama:

> "Elimu huzuia kuibuka na kukua kwa uhalifu katika jamii, Elimu huondoa umaskini katika jamii, …elimu kujenga jamii yenye maadili mazuri" (*Watoto wa Mama N'tilie*)

Katika riwaya ya "*Takadini*' alitoa hoja kama vile:-,

> "Elimu ni muhimu katika kutokomeza mila potofu, elimu inahitajika kuhusu athari za ndoa za kulazimishwa na umuhimu wa elimu katika kujikimu kimaisha na kuendeleza jamii".

Aidha mtahiniwa huyo alitoa maelezo mazuri katika kufafanua hoja zake na kutoa hitimisho zuri linalowiana na swali. Kielelezo 13.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua vizuri kuhusu umuhimu wa elimu katika riwaya mbili teule.

**Kielelezo 13.2**

13. ..Elimu ni mafunzo na maarifa ambayo
mtu hupata au hupokea katika kwa wakati na mazingira
yanayomzunguka. Katika riwaya zetu, tunaweza
kuona vyema jinsi wasanii wanavyoonesha umuhimu
wa elimu katika jamii. Katika riwaya ya "TAKADINI"
pamoja na riwaya ya "WATOTO WA MAMAN'TILIE",
wasanii wanaonesha kuwa, elimu ni ufunguo wa
maisha katika namna ifuatavyo;

Kwa kuanza na riwaya ya "WATOTO WA
MAMAN'TILIYE" iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo,
mwandishi anaeleza yafuatayo kuhusu elimu;

Elimu huzuia kuibuka na kukua kwa
uhalifu katika jamii. Katika riwaya hii mwandishi
anaonesha suala hili kwa kupitia wahusika Peter
na Musa ambao kutokana na umasikini, wanakosa
elimu ya kwenda shule na kuamua kuingia katika
makundi ya madawa ya kulevya na wizi. Endapo
kama wahusika hawa wangepata elimu, basi wangewe-
za kutambua madhara yaliyopo katika uhalifu. Watoto
hawa wanafukuzwa shule na mwalimu akisema,

"Wale wote wasio na ada na sare za shule,
hakuna shule..."

13. Hivyo basi, elimu ni ufunguo wa maisha kwa huepusha uhalifu na kuleta usalama katika jamii.

Elimu huondoa umasikini katika jamii; Hili linazungumziwa vyema kwa kupitia muhusika Mzee Lomolomo ambaye kutokana na ukosefu wa elimu na maarifa, anajiingiza katika ulevi na kutelekeza familiya yake hata kushindwa kutumia hakiba yao yositu. Anasema "...Leo ntatafuta hakiba yao ya siku.. kisha nielekee bungeni..." mwandishi pia anasema "...Mzee Lomolomo kwake yeye gongo na pombe ya matapitapu alivifanya dini..."

Hivyo, ukosefu wa elimu unaleta umasikini kama inavyoonekana katika familiya ya Mama n'tilie na Mzee Lomolomo ambaye anafariki kutokana na ulevi.

Mwandishi pia anaonesha pia umuhimu wa elimu katika kujenga jamii yenye maadili mazuri. Muhusika Zenabu anaonekana kukosa elimu na hivyo kufanya mambo ambayo yanaharibu maadili ya watoto wanaomtazama. Mwandishi anasema,

"Zenabu alichukua kiberiti na kuwasha sigara... Peter alimtazama jinsi moshi mwingi ulivyotoka puani na mdomoni..."

Hivyo, elimu inahitajika kwa kiasi kikubwa ili kujenga jamii iliyo bora.

Katika kitabu cha "TAKADINI" kama kilivyoandikwa na Ben J. Hanson, mwandishi ameonesha umuhimu wa elimu kama ifuatavyo:

Elimu ni muhimu katika kutokomeza mila potofu. Katika kitabu hiki mwandishi anaonesha uwepo wa mila potofu kama mauaji ya albino kwa kupitia muhusika Takadini ambaye anatokea kutaliwa tangu akiwa mtoto mdogo

13. Kulingana na ulemavu wake wa ngozi. Muhusika Ziki anasema, "Kulingana na mila za mababu zetu katika kila koo na kijiji, watoto wenye ulemavu wa ngozi lazima wauawe, walio walemavu lazima wauawe na pacha mmoja lazima auawe..."

Hivyo, mwandishi anaonesha kwamba elimu inahitajika sana ili kuweza kuziondoa mila hizi potofu zilizopo katika jamii kwani hazina umuhimu wowote.

Elimu inahitajika kuhusu athari za ndoa za kulazimishwa. Katika riwaya hii, tunaona muhusika Shingai akilazimishwa kuolewa na Nhamo wakati yeye anampenda Takadini. Anasema,

"Amai, si ya kwamba sipendi kuolewa na Nhamo, lahasha! Lakini sidhani kama nitakuwa na furaha nikiwa naye..." Suala hili linazusha ugomvi kutokana na ukosefu wa elimu kuhusu kumpa binti haki ya kuchagua.

Mwandishi pia ameonesha umuhimu wa elimu katika kujikimu kimaisha na kuiendeleza jamii. Hili linaonekana kupitia muhusika Takadini ambaye anapokea elimu ya dawa za miti shamba kutoka kwa Chivero jambo linalomfanya aweze kuwa mtu bora na muhimu kijijini hapo baada ya kufariki kwa mganga bingwa, Mzee Chivero. Hii inaonesha wazi ya kuwa elimu ni ufunguo wa maisha kwani hukuza vipaji na maarifa katika jamii.

Hivyo basi, kwa kuhitimisha, tumeweza ona ukweli uliopo katika msemo ya kwamba 'Elimu ni ufunguo wa maisha' katika riwaya hizi mbili katika masuala ya kifamilia na kiutamaduni katika jamii kama hali halisi iliyopo katika maisha yetu, hivyo, elimu ipewe kipaumbele kwa maendeleo ya jamii.

Kielelezo 13.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kufuata matakwa ya swali.

Watahiniwa wachache (18.20%) walipata alama dhaifu 0 hadi 4 kwa kuwa walitoa majibu yasiyo sahihi kwa hoja nyingi. Baadhi ya watahiniwa walijadili dhamira mbalimbali zilizopo katika riwaya husika badala ya kufafanua usemi “Elimu ni ufunguo wa maisha” kwa kuonesha umuhimu wa elimu katika kupambana na changamoto mbalimbali za maisha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika riwaya ya “*Watoto wa Mama N’tilie”* alielezea dhamira kama vile “ndoa” na alishindwa kabisa kufafanua jinsi gani elimu ni ufunguo wa maisha katika kutatua changamoto za kutokuwepo kwa mapenzi ya dhati katika ndoa. Vilevile, katika aya ya kwanza na ya pili mtahiniwa huyo alitoa majibu yasiyojitosheleza kwa kushindwa kuonesha ni kwa namna gani elimu ilivyoondoa *umaskini* na *imani potofu* katika jamii. Kielelezo 13.3 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini katika swali hili.

**Kielelezo 13.3**

13. "Elimu ni ufunguo wa Maisha" Fafanua...
kauli hii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu
kati ya vitabu viwili uya niwaya vilivyoorodheshwa

Elimu - Ni uwasilishaji wa ujuzi kutoka sehe
mu kwenda sehemu nyingine au jamii moja kuen
da jamii nyingine. Pia katika kitabu cha "TAKA
DINI" mwandishi Ben J. Hanson na Kitabu cha
"WATOTO WA MAMANTILIE" Mwandishi ana
eleza kuwa elimu ndio kitu kinaweza kupati
a ajila Mwanadamu. Pia elimu tunaweza kupa
ta faida mbalimbali ambazo ni;

Umaskini; Ni hali ya mtu kukosa vitu vya
muhimu kama vile chakula, Mavazi na Elimu. Pia kat
ika jamii yetu ya Tanzania, watu wengi waku
wana Maisha Magumu kwa sababu ya ukosefu
wa elimu. Mfano, Mwandishi amemtumia
Mzee Makwati alikuwa na wake wanne, ambap
apo alipelekea kutokea kuna Maisha Magumu.

Imani Potofu; Ni hali ya mtu kuamini,
Mungu ambayo inapelekea kutokea kwa migo
goro katika. Hii yote hupelekea kuwa ukosefu
wa Elimu. Katika jamii hizo. Katika jamii za kitanz
ani watu wengi wakiamini imani za kishirikina
mfano Mwandishi amemtumia Mzee Makwati
kama mzee alikuwa akiamini imani za kishirikina
na kuzua migogoro katika jamii yake

Ndoa; ~~Kuna~~ Ni hali ya makubaliano yana
yo juu ya watu wawili kuishi pamoja. Katika
jamii yetu ya Kitanzania ~~kakuna~~ mapenzi
ya dhati na Mapenzi ya dhati.

Kielelezo 13.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vibaya na kupata alama chini ya wastani.


### 2.5.4 Swali la 14: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Andishi* (*Uhakiki wa Tamthiliya*) na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kumtumia mhusika mmoja kwa kila tamthiliya na kutoa hoja tatu kwa kila mhusika kuthibitisha kuwa "wahusika katika kazi ya fasihi ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao" kupitia tamthiliya mbili alizosoma. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 179,725 sawa na asilimia 56.58 kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 69.56 walijibu vizuri na kupata alama za juu na za wastani.

Watahiniwa wengine (69,608) sawa na asilimia 38.73 walijibu swali hili na kupata alama za wastani 4.5 hadi 9.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa hoja nyingi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa utangulizi usiojitosheleza kwa kuandika majina ya vitabu vya Tamthiliya kwa herufi ndogo na pia alikuwa na shida ya kitahjia ambapo hakuandika kwa usahihi maneno mengi. Katika kiini mtahiniwa huyo alitaja hoja sahihi lakini maelezo ya hoja zake hayakujitosheleza kwani alitaja wasifu chanya wa wahusika bila kueleza jamii inajifunza nini kutoka kwao. Aidha, hitimisho lake lilikuwa na kauli ya kupingana na matakwa ya swali, kama vile:- *"Wahusika kwenye kazi ya fasihi huweza kuwa na tabia na matendo mabaya au mazuri"* badala ya kuelezea jinsi wahusika katika kazi ya fasihi walivyo mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao mema. Kielelezo 14.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 14.1**


Katika jamii mtu a elimu ni fungo wa maisha sababu kukiwa na helimu kwenye kijiji watu huishi kwa amani na nimaendeleo kwao.
Kutoroka na ngowe aliamua kuchoma na ripoti Ngowe alisongwesha. pia kwenye tamthilia ya kilio chetu.
Mama suzi alikuwa na tabia nzuri na pia alikuwa mama wa familia aliweka familia yake katika hali nzuri kama mama wa familia.
Alishauli mwanaye ~~Mazo~~ suzi, mama ~~mazo~~ suzi alimshauli mto wake ~~mazoo~~ a suzi kuhusu mapenzi na shule ingawa suzi akasibilia ushauli wake.
pia Mama suzi alikuwa mtu mwenye ukali kidogo, ukali unaoingia huwaidia kupambana na vijana vibaya katika Jamii.
~~Kwa~~ Wahusika kwenye kazi ya fasihi huweza kwa na tabia na matendo mabaya au mazuri.

Kielelezo 14.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutoa hoja sahihi lakini maelezo katika hoja zake hayakujitosheleza. Aidha mtahiniwa alikuwa na tatizo la kitahjia kwa maneno mengi. Mfano, ‘alishauli’ badala ya kuandika *alishauri.*

Kiasi cha watahiniwa 55,402 sawa na asilimia 30.83 walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu 10 hadi 15. Watahiniwa hao waliweza kuthibitisha kuwa wahusika katika kazi za fasihi ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao na waliweza kutoa hoja tatu kwa kila mhusika katika tamthiliya mbili walizosoma. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa utangulizi na hitimisho zuri, na katika kiini aliweza kutoa wasifu wa mhusika *Anna* katika tamthiliya ya “*Kilio Chetu*” kama vile:- *“muelimishaji rika, mwenye msimamo, mwenye huruma na upendo”*. Kwa upande wa tamthiliya ya “*Orodha*”, akamwelezea mhusika *Mama Furaha* na kama: *“mtu mwenye upendo wa dhati kwa watoto wake, mwaminifu na mtekelezaji….* Aidha, alionesha jinsi wahusika hao wanavyofaa kuigwa na jamii kwa tabia

na matendo yao. Kielelezo 14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 14.2**

14. Wahusika katika kazi za fasihi ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao. Wahusika ni viumbe wanaotumika na waandishi ili kufikisha ujumbe na dhamira fulani. Kwa kutumia "KILIO CHETU" cha Medical Aid Foundation na tamthiliya ya "ORODHA" ya Steve Reynolds kuthibitisha kauli hii.

Kwa kuanza na "Kilio Chetu" mhusika Anna anafaa kuigwa na jamii kwani ni muelimishaji rika. Anna anaonekana akimweleza Mwarami juu ya magonjwa ya zinaa ili aweze kuepuka naye kwani Mwarami ~~alit~~ anataka kujihusisha kimapenzi na Anna. Anna anasema,

"Hujui magonjwa ya zinaa wewe? Kisonono, kaswende na mengine kedekede.
Haya hata juu ya UKIMWI hujui? ----"

Mhusika Anna anafaa kuigwa katika jamii. Katika jamii zetu kuna watu kama Anna wanaoelimisha rika.

Aramsimamo. Anna ni mhusika mwenye msimamo. Anaonekana kukataa uhusiano na Mwarami kwani umri hauruhusu na bado anasoma. Anaonekana kutokushawishika na wanaume wa aina yoyote, wenye mali nyingi na magari. Anabaki na msimamo wake wa kutokujihusisha na mapenzi katika umri mdogo. Hii inamsaidia kutokupata mimba na ~~u~~ magonjwa.

Mama Furaha anasema,

"Yupo anaosha vyombo, ntaongea nae..."

Mama Furaha ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yake.

Kwa kuhitimisha, wahusika katika kazi za fasihi ni mifano ya kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao. Wahusika wametumika katika njia ya kuonya madhara na kuendeleza tabia nzuri katika jamii.

Kielelezo 14.2 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kuthibitisha kuwa wahusika katika kazi za Fasihi ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao kwa kumtumia Anna na Mama Furaha.

Aidha, watahiniwa 69,608 sawa na asilimia 30.44 walijibu vibaya swali hili na kupata alama dhaifu 0 hadi 4 kwa kuwa walishindwa kutumia mhusika mmoja kutoka katika kila tamthiliya mbili walizosoma kuthibitisha kuwa wahusika hao ni mfano wa kuigwa na jamii kwa tabia na matendo yao. Watahiniwa hao hawakuelewa matakwa ya swali ipasavyo na hivyo baadhi yao, asilimia 7.0 walipata 0 kutokana na kuelezea wahusika wasikuwepo katika tamthiliya husika au kueleza dhamira mbalimbali bila kuhusisha wahusika. Aidha, wengine walitumia wahusika zaidi ya mmoja kutoka katika tamthiliya moja pekee na hivyo kupata alama dhaifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika utangulizi wake aliandika kuwa atatumia tamthiliya mbili "*Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe*" na " *Kilio Chetu*", bali katika majibu yake aliwatumia wahusika Ngoswe na Mazoea kutoka katika tamthiliya ya "*Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe*". Vile vile mtahiniwa huyo alitoa hitimisho lisilo sahihi kwa kutoa suluhisho la dhamira ya mapenzi badala ya kuonesha ni jinsi gani tabia na mienendo ya wahusika inavyofaa au isivyofaa kuigwa na jamii. Kielelezo 14.3 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyetumia wahusika wawili kutoka katika tamthiliya moja kinyume na matakwa ya swali.

**Kielelezo 14.3**

14 Kwa kutumia tamthiliya mbili ambazo ni NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE pamoja na tamthiliya ya KILIO CHETU kwa kutoa wasifu wa wahusika. Mhusiki ni mtu au kiumbe chochote kilicho hai na kisicho hai kinacho vaa uhusika wa kitu fulani.

Nikianza na kitabu cha "Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe" kilicho andikwa na msanii Emmanuel Semzaba. Kama ifuatavyo.

Ngoswe, huyu ni muhusika mkuu katika tamthiliya hii ya "ngoswe penzi kitovu cha uzembe. Ni kijana aliyetoka mjini kwenda kijijini kwa lengo la kuchukua idadi kamili ya wananchi kwa lengo la maendeleo ya nchi.

Ana ujuzi wa elimu, kijana ngoswe ana ujasiri na ujuzi mkubwa wa elimu ndio maana Serikari ilimchagua na kumtuma kijijini kwa lengo la kuchukua idadi ya watu yaani (Sensa)

Hana msimamo, ngoswe katika kazi aliyo tumwa kijijini hakuizingatia hatimaye akajihusisha na mambo mengine ya mapenzi na kusahau kazi au nini alicho kifuata katika kijiji hicho. hatimaye Daftari za kazi kupotea na kurudi mjini bila majibu kamili

alitaka kumtorosha mazoea, tabia ya kijana huyu haikuigarwa katika jamii kwa sababu alitaka kumtorosha binti wa mzee ngengemkeni mitomingi kwa nia

| | |
|---|---|
| 14 | ya Kumpeleka Mjini hatimaye wazazi |
| | wa binti Mazoea Kuwaona na Kukimbia |
| | Mazoea, ni binti wa barozi mzee |
| | ngengemkeni Mitomingi na ni Mtoto pia wa |
| | Mama Mazoea. |
| | hana mapenzi ya dhati, Mazoea katika |
| | Kitabu cha "ngoswe penzi Kitovu cha |
| | uzembe Msanii amempa uhusika kama |
| | binti asiye na mapenzi ya dhati kwa |
| | sababu binti mazoea alikuwa msaliti |
| | mchumba aliyetoa posa na anayepata |
| | mika kwa wazazi kumuacha na kumpeleka |
| | ngoswe. |
| | alikubali kutoloshwa na ngoswe, huyu |
| | ni binti aliye shawishiwa na kukubali |
| | ka kutoroshwa na ngoswe kwa lengo la |
| | kwenda mjini bila ya wazazi wake |
| | kufahamu hivyo tabia yake mama |
| | wazo yake haya ku yapendeza |
| | wazazi wake. |
| | Hakutaka kuwasikiliza wazazi, Mazoea |
| | alikuwa na tabia ya kufanya vitu |
| | kwa kujificha jificha hivyo ata waza |
| | zi wake alikuwa waki mshauli ku |
| | fanya mambo mazuri rakini hakuwa |
| | sikiliza na kuwa puuzia. |
| | Nahitimisho kwa kusema, si vyema |
| | kuchanganya mapenzi na kazi pia |
| | kufanya kitu kwa kufuata ushauri |
| | ni bora kuliko kujichukulia maamuzi. |

Kielelezo 14.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali kinyume na matakwa ya swali.

### 2.5.5 Swali la 15: Utungaji wa Kazi za Kifasihi

Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji wa Kazi za Kifasihi* katika mada ndogo ya *Kanuni za Utungaji wa Mashairi*. Swali lililenga kupima uundaji na lilimtaka mtahiniwa kutunga shairi la kimapokeo la kumuaga rafiki yake aliyehamia shule nyingine na lilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote waliofanya mtihani kwa kuwa lilikuwa ni la lazima. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 70.50 ya watahiniwa walipata alama za juu na za wastani. **Jedwali Na. 3** linaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.

**Jedwali Na. 3**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

| Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|
| 0.0 - 4.0 | 93,717 | 29.50 |
| 4.5 - 9.5 | 95,973 | 30.21 |
| 10.0 - 15.0 | 127,972 | 40.29 |


Watahiniwa 127,972 sawa na asilimia 40.29 walijibu vizuri kwa kuweza kutunga shairi la kimapokeo la kumuaga rafiki anayehamia shule nyingine na kupata alama 10 hadi 15. Watahiniwa hao waliweza kutunga shairi kwa kuzingatia kichwa cha shairi kilichoandikwa kwa herufi kubwa, urari wa vina na mizani, mishororo na idadi ya beti kama ilivyotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga kwa usahihi ubeti ufuatao;

*"Mwishoni namalizia, adabu ushikilie,*
*Ukweli nakuambia, magumu uvumilie,*
*Neema takufikia, muumba mshikilie*
*Rafiki yangu mpendwa, nenda kasome salama"*

Hivyo, ubeti huo na nyingine alizotunga zilikuwa na utoshelevu wa vina, mizani 16 kwa kila mstari na idadi ya beti ambazo ni nne kama ilivyotakiwa. Aidha, mtahiniwa huyo aliweza kuzingatia mawazo makuu kutokana na kichwa cha shairi alichopewa katika beti zote nne kwa lengo la kumuaga rafiki yake anayehamia shule nyingine. Pia,

alitumia lugha nzuri ya kishairi na lugha ya mkato ili kulifanya shairi liweze kuimbika. Kielelezo 15.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga shairi kwa kuzingatia sheria na kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo.

**Kielelezo 15.1**


15. RAFIKI YANGU ANAYEHAMIA SHULE NYINGINE.

1. Rafiki ninaongea, hamaza nakupatia,
Naamini tapokea, Vizuri utazikia,
Popote tapokosea, ni vyema kuulizia,
Rafiki yangu mpendwa, kasoma tena salama.

2. Mwalimu msikiliza, mwangaza takupatia,
Naomba usipuuze, matatani kuingia,
Bidii usipunguze, ushindi tafurahia,
Rafiki yangu mpendwa, kasoma tena salama.


3. Tabaki kituombea, maarifa kupokea,
Kazi usijetegea, ndiyo yakutegemea,
Uvivu nao kemea, madhara yakuletea
Rafiki yangu mpendwa, kasoma tena salama.

4. Mwishoni namalizia, adabu ushikilie,
Ukweli nakuambia, magumu uvumilie,
Neema takufikia, Muumba mshikilie,
Rafiki yangu mpendwa, kasoma tena salama.

Kielelezo 15.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kutunga shairi la kimapokeo lililojitosheleza na kupata alama za juu.

Hata hivyo, watahiniwa 95,973 sawa na asilimia 30.21 walipata alama za wastani 4.5 hadi 9.5 kwa kuwa walitoa majibu yasiyojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitunga shairi lenye beti nne, lililozingatia vizuri kichwa cha shairi lakini hakutumia kanuni za urari wa vina na mizani na utoshelevu wa ujumbe kwa baadhi ya beti zake na hivyo kupata alama za wastani. Aidha, mtahiniwa huyo hakutumia lugha ya kishairi na yenye mvuto katika beti zake kama ilivyotakiwa. Kielelezo 15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani.

**Kielelezo 15.2**


15. "RAFIKI YANGU ANAYEHAMIA SHULE NYINGINE"

1. Nilipopata rafiki, Nahofu sikuipata
Ilikuwa nimikiki, Kutwa [illegible]
Leo kwangu mimidhiki,
Nakuombea kwa mungu, huianze salama safari

2. Uhoga umenijia, kusoma kwangu nishinda
Sina pakukimbia, Pale niwapo nashinda,
Umuitapo hana mfanowe kama dada
Sijui nitanyenini, kumpata tena rafiki

3. Huchaguapo rafiki, huwe ni msaada wako,
Hasijekuwa mnafiki, hazifue shida zako,
Husifiwashie koki, Kumueleza maisha yako
Nakuombea kwa mungu, kuanza salama safari


4. Husichoke kusubili, huta angukia pabaya
Hata kwasiku mbili, wanaclamia huwa wabaya
Hatakuchoka kimuili, atasema sula mbaya
Maisha nisharafi ndefu kutembea husichoke.

Kielelezo 15.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kutunga shairi la kimapokeo lisilozingatia kanuni na sheria za utunzi kama vile kutumia mizani pungufu kwa mfano, ubeti wa pili; mstari wa pili na wa tatu.

Kiasi cha watahiniwa 93,717 sawa na asilimia 29.50 walipata alama hafifu 0 hadi 4 kutokana na kukosa maarifa kuhusu kanuni na sheria za utunzi wa mashairi ya kimapokeo. Miongoni mwao, asilimia 18.07 walipata 0 kutokana na kushindwa kabisa kutunga shairi la kimapokeo kuhusu "Rafiki yako anayehamia shule nyingine". Baadhi ya watahiniwa walielezea mbinu anuai za utunzi wa mashairi kama vile *vina*, *mizani* na *ubeti* bila kutunga shairi kinyume na matakwa ya swali. Aidha, wengine walichambua maudhui katika vitabu teule badala ya kutunga beti nne za shairi kama ilivyotakiwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika uchambuzi wa maudhui yenye dhamira kama ."matabaka, mapenzi na ndoa, kupiga vita mkoloni, kupiga vita ukoloni mamboleo….." kutoka katika diwani teule "*Malenga Wapya*" na "*Wasakatonge*". Kielelezo 15.3 kinaonesha sehemu ya jibu la

mtahiniwa aliyeandika uchambuzi wa maudhui (dhamira) kutoka katika diwani teule badala ya kutunga shairi la kimapokeo.

**Kielelezo 15.3**


15 Mashairi, Ni utanzu wa sanaa inayokuwasilishwa
maneno fasaha, lugha ya mkato. Zifuatazo ni Tunga shai-
ri la kimapokeo lenye beti nne kuhusu. Kwa kuzingatia-
na "MALENGA WAPYA" na "WASAKATONGE", nihojadili
na ifuatayo ni "MALENGA WAPYA"
Matabaka, vita na mtaa uporaji wa wizi na ua
pala vurga kwa kulevya bangi na kulevy ya dawa ni
wawili unaweza dhaifu yoyote zurura ngumu bila usingizi
tu hapa jenga basi pia na njia hatari
Mapenzi na ndoa, vita na mtaa utapata mimba wa
usumbuaji sababu uporaji wa wizi na ua pala vurga kwa-
kulea acha na kulevya ya dawa ni wawili unaweza
dhaifu yoyote zurura ngumu bila usingizi tu hapa jenga
basi pia na njia hatari
Kupiga vita mkoloni, vita na mtaa uporaji wa wizi-
na ua pala vurga kwa kulevya bangi na kulevya ya dawa-
ni wawili unaweza dhaifu yoyote zurura ngumu bila usi-
ngizi tu hapa. Nijadili na ifuatavyo ni "WASAKATONGE"
Kupiga vita matabaka, vita na mtaa utapata vita
vya vurga usumbuaji sababu uporaji wa wizi na ua-
pala vurga kwa kulea acha na kulevya ya dawa ni wawili
unaweza dhaifu yoyote zurura ngumu
Kupiga vita ukoloni mamboleo, vita na mtaa utapa-
ta vita vya vurga kwa kulea acha na kulevya ya dawa-
ni wawili unaweza dhaifu yoyote zurura ngumu bila u-
singizi tu hapa jenga basi pia na njia hatari
Kupiga vita mkoloni, vita na mtaa utapata vita

Kielelezo 15.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyechambua maudhui katika diwani ya "*Malenga Wapya"* na "Wasakatonge" badala ya kutunga shairi kama alivyotakiwa. Hata hivyo, kifungu hicho hakikuwa na mantiki yoyote inayohusiana na diwani hizo kwa jumla.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA

Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali kumi na tano (15) yaliyotoka katika mada za *Ufahamu na Ufupisho*, *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali*, *Matumizi ya Sarufi*, *Uandishi*, *Maendeleo ya Kiswahili, Uhakiki wa Kazi za Fasihi* na *Utungaji wa Kazi za Fasihi*.

Uchambuzi wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani katika mada zote zilizotahiniwa. Kiwango kizuri cha kufaulu kilikuwa katika mada nyingi kikijumuisha *Uhakiki wa Fasihi Andishi katika Ushairi* (94.81%), *Ufahamu na Ufupisho* (87.23%), *Fasihi Simulizi* (85.51%), *Uandishi* (85.20%), *Uhakiki wa Fasihi Andishi katika Tamthiliya* (81.80%), *Kutunga Kazi za Fasihi* (70.50%) na *Uhakiki wa Fasihi Andishi katika Riwaya* (69.56%).

Aidha, mada za *Matumizi ya Sarufi* (48.05%), *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* (39.60%) na *Maendeleo ya Kiswahili* (34.50%) zilikuwa na viwango vya wastani vya kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani huu.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa 021 Kiswahili kwa mwaka 2017 kupitia mada mbalimbali kilikuwa ni kizuri. Wastani wa kufaulu kwa mada zote ni asilimia 69.68 ikiwa na ongezeko kubwa la asilimia 19.58 ikilinganishwa kiwango cha wastani cha kufaulu kwa mada kwa mwaka 2016. Hali hiyo inadhihirisha kuwa, zaidi ya nusu ya watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa mwaka 2017.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla Mtihani wa Kidato cha Nne katika somo la Kiswahili mwaka 2017 ulizingatia Muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalihusisha ngazi zote za majazi ya utambuzi yaani *maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini*. Kiwango cha kufaulu kwa jumla ni kizuri ambapo asilimia 84.42 ya watahiniwa walifaulu somo hili.

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutatuliwa kama vile kutofuatwa kwa maelekezo ya swali na uelewa mdogo wa mada mbalimbali na hasa mada za *Sarufi*, *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na *Maendeleo ya Kiswahili*. Ili kuinua zaidi kiwango cha kufaulu katika mada zote kwa mtihani wa Kidato cha Nne, mikakati mbalimbali inahitajika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Kwa mfano, mada ya *Sarufi* na *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* sharti zitiliwe mkazo zaidi katika mbinu zitumikazo kufundishia mada hizo ili kuwawezesha wanafunzi kupata ujuzi wa kujieleza kwa ufasaha na kukuza msamiati wa lugha ya Kiswahili hasa ikizingatiwa kuwa *sarufi* na *matumizi ya lugha* ndiyo msingi wa mawasiliano katika lugha. Aidha, kuhusu mada ya *Maendeleo ya Kiswahili*, jitihada zinahitajika ili kuwajengea wanafunzi ujuzi wa kutambua vyanzo vya lahaja na historia ya lugha ya Kiswahili kwa jumla ili kupata wataalam watakaokuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

Kiwango hiki cha kufaulu kinaonesha kuwa, zipo mada zinazohitaji kutiliwa mkazo katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* imeendelea kuwa na kiwango cha chini cha kufaulu kuliko mada nyingine zilizotahiniwa kwa miaka mitatu mfululizo japokuwa, kwa mwaka 2017 kiwango cha kufaulu kimepanda kwa asilimia 10 kutoka kiwango hafifu (24.5%) kwa mwaka 2016 na kuwa cha wastani (34.50%).

Aidha, kumekuwepo na kupanda kwa viwango vya kufaulu katika mada nyingi kutoka kiwango hafifu cha kufaulu kwa mwaka 2016 na kuwa kiwango cha wastani au kizuri kwa 2017. Mada hizo ni pamoja na *Uhakiki wa Fasihi Andishi – Tamthiliya* kutoka (11.6%) na kuwa (81.80%), *Fasihi Simulizi* kutoka (20.8%) na kuwa (85.51%), *Matumizi ya Sarufi* kutoka (27.2%) na kuwa (48.05%) na *Kutunga kazi za Kifasihi* kutoka (29.7%) na kuwa (70.50%) mtawalia.

Mwisho taarifa hii ya uchambuzi kuhusu majibu ya watahiniwa itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Kiswahili na kutatua changamoto kwa walimu na wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hali hii itawafanya walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa mbalimbali yanayosababisha kufaulu kwa kiwango cha chini ili kuweza kufanya marekebisho kwa ajili ya kuinua kiwango cha kufaulu kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuongeza kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika somo la Kiswahili, mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa;

(a) Wanafunzi wazoeshwe kufanya utafiti katika lugha zao za asili na lugha ya Kiswahili ili wapate maarifa ya kutosha kuhusu vyanzo vya lugha mbalimbali na tofauti zinazoweza kubainishwa katika lugha moja na nyingine.

(b) Wanafunzi wasisitizwe kutumia sarufi sahihi ya Kiswahili ili kujijengea weledi katika mada ya *Matumizi ya Sarufi* na *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* ili kuondokana na tatizo la matumizi ya lugha kisarufi yasiyokuwa sahihi.

(c) Wanafunzi wahamasishwe kujihusisha na utunzi wa kazi za fasihi hususan mashairi ya kimapokeo na vipera vya Fasihi Simulizi kwa ujumla. Pia wajengewe ujuzi wa kuweza kutunga kazi hizo ambazo zitaleta tija katika kupata watunzi bora wa fasihi simulizi.

(d) Kutiliwe mkazo zaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote hususani mada za *Sarufi*, *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali*, *Maendeleo ya Kiswahili na Utungaji wa Kazi za Kifasihi*. Aidha, wanafunzi wahamasishwe kusoma vitabu vya kiada na ziada na kufanya mazoezi mbalimbali yanayohusiana na mada hizo.

**KIAMBATANISHO A**

## UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

| Na | Mada | 2017 | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya maswali | Asilimia ya Watahiniwa Waliopata Wastani wa Asilimia 30 au Zaidi | Maoni |
| 1 | Uhakiki wa wa Fasihi Andishi - Ushairi | 12 | 94.81 | Vizuri |
| 2 | Ufahamu na Ufupisho | 1, 2 | 87.23 | Vizuri |
| 3 | Fasihi Simulizi | 11 | 85.51 | Hafifu |
| 4 | Uandishi | 8, 9 | 85.20 | Vizuri |
| 5 | Uhakiki wa Fasihi Andishi - Tamthiliya | 14 | 81.80 | Vizuri |
| 6 | Kutunga Kazi za Fasihi | 15 | 70.50 | Vizuri |
| 7 | Uhakiki wa wa Fasihi Andishi - Riwaya | 13 | 69.56 | Vizuri |
| 8 | Matumizi ya Sarufi | 3, 4, 7 | 48.05 | Wastani |
| 9 | Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali | 5, 6 | 39.60 | Wastani |
| 10 | Maendeleo ya Kiswahili | 10 | 34.50 | Wastani |

**KIAMBATANISHO B**

## ULINGANIFU WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2016/2017

| S/N | MADA | Idadi ya Maswali | 2016 | | 2017 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Asilimia ya watahiniwa waliopata wastani wa alama 30 na zaidi | Maoni | Asilimia ya watahiniwa waliopata wastani wa alama 30 na zaidi | Maoni |
| 1 | Uhakiki wa wa Fasihi Andishi - Ushairi | 1 | 69.1 | Vizuri | 94.81 | Vizuri |
| 2 | Ufahamu na Ufupisho | 2 | 80.6 | Vizuri | 87.23 | Vizuri |
| 3 | Fasihi Simulizi | 1 | 20.8 | Hafifu | 85.51 | Vizuri |
| 4 | Uandishi | 2 | 87.5 | Vizuri | 85.20 | Vizuri |
| 5 | Uhakiki wa Fasihi Andishi - Tamthiliya | 1 | 11.6 | Hafifu | 81.80 | Vizuri |
| 6 | Kutunga Kazi za Fasihi | 1 | 29.7 | Hafifu | 70.50 | Vizuri |
| 7 | Uhakiki wa wa Fasihi Andishi - Riwaya | 1 | 88.5 | Vizuri | 69.56 | Vizuri |
| 8 | Matumizi ya Sarufi | 3 | 27.2 | Hafifu | 48.05 | Wastani |
| 9 | Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali | 2 | 61.5 | Wastani | 39.60 | Wastani |
| 10 | Maendeleo ya Kiswahili | 1 | 24.5 | Hafifu | 34.50 | Wastani |